يقين
YAQEEN
مكتب الدعوة والإرشاد بالمعذر وأم الحمام



باللغة السواحيلية

# التوحيد الميسر

# TAUHIDI ILIYO NYEPESI


Mtunzi: Sheikh Abdullah bin Ahmed Al Hwail
Mfasiri: Sheikh: Yasini Twaha
Kimerejewa na Sheikh: Yunus Kanuni Ngenda

عبد الله بن أحمد الحويل
مترجم الشيخ: ياسين طه
محقق الشيخ: يونس كنون نغندا

التوحيد الميسر

تأليف
عبد الله بن أحمد الحويل

مترجم الشيخ: ياسين طـه

محقق الشيخ: يونس كنون نغندا

# TAUHIDI NYEPESI

Mtunzi: Sheikh
Abdullah bin Ahmed Al Hwail

Mfasiri: Sheikh:
Yasini Twaha
Kimerejewa na Sheikh:
Yunus Kanuni Ngenda

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Tunamshukuru Allah Mlezi wa Ulimwengu mzima, na Rehma na Amani za Allah zimuendee wa Mwisho wa Mitume Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), pamoja na Familia yak e na Maswahaba zake na Waislamu woote watakaofuata mwenendao wake hadi siku ya qiyama. Amma baad:

Haya ni maneno machache yenye manufaa, na mambo mbali mabali yalio kusanywa, na faida za hali yajuu, katika mlango wa (Tauhidi). Tauhidi ambayo hakubali Allah matendo yasio kuwa na Tauhidi, na wala hawi radhi na mja isipokuwa atapo hakikisha Tauhidi.

Nimekusanya ndani ya maneno haya (dondoo Fupifupi). Vidhibiti na Kanuni na Vigawanyo, vinamkusanyia msomaji vilivyo sambaa, na vinamuwekea udhibiti wa vilivyo kimbia, na humpangilia Elimu katika Akili yake.

Na ilivyokua katika (jambo lolote) halijulikani isipokuwa utakapojua mambo mawili:
1- Hakika yake.
2- Kubainisha kinyume chake.

Nimefanya pupa katika kuweka wazi uhakika wa (Tauhidi) na kubainisha asili yake na vigawanyo vyake, kisha nikataja (Kinyume cha Tauhidi) nayo ni (Shirki), nikaielezea nikaweka wazi namna zake na aina zake na hukumu zake.
kwa sababu: Kinyume cha mambo hudhihirisha uzuri wake na kinyume cha mabo vitu huwa wazi.

Huwezi kujuwa uzuri wa Tauhidi na ubora wake ila baada ya kujuwa Ubaya wa Ushirikina na hatari zake, na kwa hakika nimekusanya katika dondoo fupi hizi mambo mengine ambayo nilazima Mcha Allah ayajuwe.

Kwa hakika nimejitahidi kupangilia mambo na kuyakusanya na kuyagawa, nikajihimiza katika mambo ya sheria na maana zake pamoja na kutaja dalili kwa kifupi ili iwe (Ndondoo) nyepesi kuhifadhi na kuelewa.

Nimejiepusha na kurefusha kunako chosha, na kufupisha kusiko na faida, nimejaalia Risala hii kuwa ya (Kati kwa kati), ikiwa nimepatia basi ni kwaajili ya Allah pekeyake, na ikiwa nimekosea nikwa sababu ya nafsi yangu pamoja na Shetani.

Kwa hakika nimekusanya hizi (Ndondoo) kutoka kwenye vitabu vya wanachuoni wenye kumcha Allah wajulikanao,

Na nikakiita (TAUHIDI NYEPESI).
Nina muomba Allah muweza wa kila jambo awanufaishe kwa kitabu hiki, na ajaalie kiwe katika mizani ya mema yangu siku ya kukutana nae.
Rehma na Amani za Allah zimuende nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), pamoja na Familia yake na Maswahaba zake na Waislamu wote watakaofuata mwenendo wake hadi siku ya mwisho.

# MAANA YA TAUHIDI

***Kilugha:** Ni chimbuko alifanya kitu kimoja anafanya kitu kimoja atakapo jaalia kikawa kimoja.

***Mifano**: utakaposema: Asitoke ndani ya nyumba yeyote isipokuwa Muhammad.

Utakuwa umemuhusisha Muhammad pekeyake kutoka ndani ya nyumba. Na utakaposema: Asisimame yeyote katika kikao isipokuwa Khalid pekeyake. Utakuwa umemuhusisha Khalid pekeyake kusimama.

***Kisheria:** Kumpwekesha Allah katika:

1- Rubuubiyya.
2- Uluuhiyya.
3- As'mau wa swifati.

# VIGAWANYO VYA TAUHIDI

Imegawanyika Tauhidi katika vigawanyo vi tatu:
1- Tauhidi Rubuubiyya.
2- Tauhidi Uluuhiyya.
3- Tauhidi As'mau wa swifati.

NIJUU YAKO KUFAHAMU KILA KIGAWANYO PAMOJA NA KUBAINISHA DALILI ZAKE

| Namna ya Tauhidi | Maana yake | Dalili yake |
|---|---|---|
| Tauhidi Rubuubiyya | Kumpwekesha Allah Mtukufu kwa:<br>1- Kuumba.<br>2- Na Ufalme.<br>3- Na Uendeshaji.<br>Au tunasema: kumpwekesha Allah Mtukufu kwa vitendo vyake. Mifano ya vitendo vyake: kuumba, kuruzuku, kuhuisha, kufisha, kuteremsha mvua, na kuotesha miti.. na mengineyo. | (Fahamuni! Kuumba na amri ni zake).<br>(Na Allah ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi).<br>(Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yasimamia mambo yote? Watasema: Allah, Allah. Basi sema:Je! Hamchi?). |
| Tauhidi Uluuhiyya<br>(Huitwa: Tauhidul-Ibada ) | Nayo ni kumpwekesha Allah Mtukufu kwa vitendo vya waja. Mifano yake: kama swala, na funga, na hijja, na kutegemea, na nadhiri, na khofu, na kutaraji, na mapenzi… na mengineyo. | (Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi).<br>(Muabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote).<br>(Na hatukutuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana Allah isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu). |
| Tauhidi As'mau wa swifati | Nayo ni kusifiwa Allah kama alivyo jisifu mwenyewe na kama alivyo sifiwa na Mtume wake (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake) kwa sifa za ukamilifu bila ya kusema: Ni kaifia fulani, au namna Fulani, au kuzipindisha, au kuzikataa. | (Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona).<br>(Na Allah ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda). |

## FAIDA MUHIMU

1: Vigawanyo vya Tauhidi ni vitatu vyenye kushikana, kila namna haiachani na nyingine, yeyote atakae leta namna Fulani akaacha nyingine huyo atakuwa sio Mwenye kumpwekesha Allah.

2: Yatakiwa ufahamu ya kwamba makafiri walio pigwa vita na Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), walikuwa wanakiri Tauhidi Rubuubiyya, wao wanakiri ya kwamba Allah ndie muumbaji mtoa rizki, Mwenye kuhuisha na kufisha, Mwenye kunufaisha na kudhuru, ambae anaendesha mambo yote.. hilo halikuwaingiza katika Uislamu,
na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yasimamia mambo yote? Watasema: Allah, Allah. Basi sema:Je! Hamchi?). (Yunus: 31).

3: Tauhidi uluuhiyya ndiyo mada ya Mitume, kwa sababu yenyewe ndio msingi ambao hujengewa juu yake amali zote, na bila kuihakikisha matendo yoote hayakubaliwi, kwa sababu kama haikuhakikishwa hupatikana kinyume chake nayo ni Shirki, na ugonvi kati ya Mitume na nyumati zao mzunguko ulikuwa katika Tauhidi hii, niwajibu kuitilia umuhimu na kusoma mambo yake na kufahamu misingi yake

## UMUHIMU WA TAUHIDI NA FADHILA ZAKE

**1: Tauhidi ndio nguzo kubwa ya Uislamu.**
Na ndio jambo lake kubwa lakulingania, wala haiwezekani kwa Mtu kuingia katika Uislamu ila atapo shahidilia Tauhidi, na akakiri kuabudiwa Allah na akakanusha yote  yasiyo mfaa Allah.

Kasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: *kushahidilia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu, nakushahidilia ya kwamba Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake) ni Mtume wake.

*Na kusimamisha Swala.
*Na kutoa Zaka.
*Na kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani.
*Na kwenda Hijja). kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

**2: Tauhidi ndio jambo muhimu katika mambo muhimu, na ndio wajibu wa kwanza.**

Ndio yenye kutangulizwa katika kila matendo, na yenye kutangulia kila jambo muhimu, kutokana na daraja yake kubwa, na umuhimu wake mkubwa.

Na ndio jambo la kwanza analo linganiwa mja, Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kumwambia Muadhi (Radhi za Allah ziwe juu yake) alipo mtuma Yemen: (Hakika wewe unawaendea watu walio pewa kitabu, liwe jambo la kwanza kuwalingania: Kushahidilia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu). Na katika upokezi mwengine: (Wampwekeshe Allah). kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

**3: Ibada hazikubaliwi isipokuwa ziwe na Tauhidi.**

Tauhidi ni sharti ya kusihi Ibada, na ndiyo msingi wa kukubaliwa kwake, na Ibada haitambuliki kama Ibada isipokuwa ikiwa na Tauhidi, kama vile Swala haitambuliki isipokuwa kwa Twahara, itapo ingia Shirki huaribika Ibada, kamavile Najsi inapoingia kwenye Twahara, na Ibada bila ya Tauhidi inageuka kuwa Shirki inaharibu matendo na huyabomowa, na hujaalia muhusika kuishi Motoni milele.

**4: Tauhidi ndio sababu ya amani na utulivu duniani na akhera.**

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka). (Al-An'aam: 82). Na makusudio ya dhulma hapa ni Shirki kama alivyo bainisha Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake). Bukhari (2/484) Hadithi ya Ibn Mas'udi (Radhi za Allah ziwe juu yake).

Amesema Ibn Kathir (r.h):
(Maana yake: Hao ambao wametakasa Ibada zao kwaajili ya Allah pekeyake asiye kuwa na Mshirika, na wala hawakumshirikisha na chochote, hao ndio wenye amani siku ya kiyama, walio ongoka duniani na akhera. Yeyote atakae leta Tauhidi ilio kamilika atapata amani ilio timia, na uongofu ulio timia, na ataingia Peponi bila ya adhabu).
Na Shirki ndio dhulma ya hali ya juu,
na Tauhidi ndio uadilifu wahali yajuu.

**5: Tauhidi ni sababu ya kuingia Peponi na kuokona na Moto.**

Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote

atakae shahidilia ya kwamba: hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu, nakushahidilia ya kwamba Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mja wake na Mtume wake, na Issa (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mja wake na Mtume wake, na neno lake kaliweka kwa Mariyamu na ni roho kutoka kwake, na pepo ni kweli, na moto ni kweli, ataingizwa peponi na Allah kwa namna yatakavyo kuwa matendo yake). kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim. Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Hakika ya Allah ameharamisha kuingia motoni yeyote atakae sema: hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu, anasema hivyo kwa kutafuta radhi za Allah). kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

**6: Tauhidi inaokoa kutokana na matatizo duniani na akhera.**
Amesema Ibnul-Qayyim (r.h):
(Tauhidi ndio kimbilio la maaduwi zake na wapenzi wake).

1: Kuhusu maaduwi zake: Ana waokowa kutokana na matatizo ya dunia na shida zake (Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Allah kwa kumsafia ut'iifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha). (Al-Ankabut: 65).
2: Lakini wapenzi wake: Ana waokowa kutokana na matatizo ya dunia na akhera na misuko suko yake, huu ndio utaratibu wa Allah kwa waja wake, hakuna kinacho ondowa matatizo ya dunia mfano wa Tauhidi, kwa sababu hiyo ikawa dua ya kuondoa matatizo ni Tauhidi, na dua ya Nabii Yunus (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), hawezi kuiomba yeyote mwenye matatizo isipokuwa Allah humfariji kwa dua hiyo ya Tauhidi. Hakuna anae ingia katika matatizo makubwa zaidi ya Shirki, na hakuna cha kuokowa zaidi ya Tauhidi, ndio makimbilio na marejeo na kinga na uokovu kwa viumbe.

**7: Tauhidi ndio hikma ya kuumbwa Binaadamu na Majini.**
Amesema Allah Mtukufu: (Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi). (Adh-Dhariyaat: 56). Maana yake: Ili wanipwekeshe.

Hawakutumwa Mitume, wala kuteremshwa Vitabu, wala kuwekwa Sheria, wala kupatikana Uumbaji isipokuwa atakaswe Allah na Aabudiwe yeye pekeyake, kinyume na chochote.

## LA'ILAHA ILLA LLAH
## Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu

***Dalili zake:**
Kauli yake Allah Mtukugu: (Allah, na Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana Allah ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana Allah ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima). (Al-Imran: 18). Na kauli yake Allah Mtukufu: (Basi jua ya kwamba hapana Allah ila Allah). (Muhammad: 19).

***Maana yake:**
Hakuna anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.

***Maana nyingine za batili:**
1: Hakuna Mwenye kuabudiwa isipokuwa Allah. Na hili ni batili, kwa sababu itakuwa maana yake: kila chenye kuabudiwa kwa haki au kwa batili itakuwa ni Allah.

2: Hakuna Muumbaji isipokuwa Allah. Na hii nisehemu ya maana yake, lakini sio makusudio; kwa sababu laiti ingelikuwa ndio maana ya La'ilaha illa llah, pasingelitokea ugonvi kati ya Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), pamoja na watu wake, kwa sababu wao hukiri hivyo.

3: Hakuna Mwenye kuhukumu isipokuwa Allah. Na hii pia nisehemu ya maana yake, lakini haitoshi na wala sio makusudio; kwa sababu tukijaalia Allah ndiye Mwenye kuhukumu lakini akaabudiwa Mwengine haipatikani Tauhidi.

***Nguzo zake:** Nguzo mbili:
1: Kukanusha (Hapana Mola).
Yaani: kukanusha ibada zote zinazo fanywa kwa asie kua Allah.
2: Kuhibitisha (Isipokuwa Allah). Yaani: kuthibitisha ya kwamba Ibada zote ni haki ya Allah pekeyake asie kuwa na mshirika.
Dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Basi anaye mkataa Shet'ani) Huku nikukanusha, (na akamuamini Allah) Huku nikuthibitisha, (bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika). (Al-Baqara: 256).
Na kauli yake: (Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu) huku nikukanusha. (Isipo kuwa yule aliye niumba) huku nikuthibitisha. (kwani Yeye ataniongoa). (Az-Zukhruf: 26-27).

***Kipindi gani La'ilaha itamsaidia binaadamu?:**
1: Atakapo tambuwa maana yake.
2: Na akaifanyia kazi, (nako ni kuacha ibada isiyokuwa ya Allah, na kufanya ibada ya Allah pekeyake).

## SHARTI ZA LA'ILAHA ILLA LLAH

***Kuzitaja kwa ujumla:**
La'ilaha illa llah haito msaidia msemaji wake isipokuwa atakapo kamilisha sharti nane:
1: Elimu inayo pingana na ujinga.
2: Yakini inayo pingana na shaka.
3: Ikhlas inayo pingana na shirki.
4: Ukweli unao pingana na uongo.
5:Mapenzi yanayo pingana na chuki.
6: Kufuata kunako pingana na kuacha.
7: Kukubali kunako pingana na kurejesha.
8: Kukanusha vinavyo abudiwa kinyume na Allah.

***Shairi linazikusanya:**
Elimu yakini na Ikh'lasi na ukweli pamoja na
Mapenzi na kufuata na kukubali hilo
Zidisha la nane yake nalo ni kupinga kwako yale
Yasiyo Allah kutokana na masanamu yaliyo geuzwa miungu.

***Kutaja masharti kwa urefu:**
**1: Elimu inayo pingana na ujinga.**
Maana yake: Elimu kwa maana ya La'ilaha illa llah kukanusha na kuthibitisha.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Basi jua ya kwamba hapana Allah ila Allah). (Muhammad: 19).

**2: Yakini inayo pingana na shaka.**
Maana yake: Msemaji awe ni mwenye yakini ilio kamilika, yakuwa Allah ndiye Mwenye kuabudiwa kwa haki.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Hakika Waumini ni wale walio muamini Allah na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Allah kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli). (Al-Huj-rat: 15).

**3: Ikhlas inayo pingana na shirki.**
Maana yake: Kuzitakasa ibada zote kwa ajili ya Allah pekeyake, na wala kisifanyike chochote kwa asie kua Allah.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:

(Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu). (Al-Bayyinah: 5).

**4: Ukweli unao pingana na uongo.**
Maana yake: Useme neno la Tauhidi haliyakua ni mkweli kwa hilo, moyo wako uende sambamba na ulimi wako.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Alif Lam Mim (A.L.M)* Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe?* Hakika tuliwajaribu walio kuwa kabla yao, na kwa yakini Allah atawatambulisha walio wa kweli na atawatambulisha walio waongo). (Al-Ankabut: 1-3).

**5:Mapenzi yanayo pingana na chuki.**
Maana yake: Kusema neno hili haliyakua unampenda Allah na Mtume wake (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na kupenda neno hili nayale yanayo onyesha juu yake.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Allah. Wanawapenda kama kumpenda Allah. Lakini walio amini wanampenda Allah zaidi sana). (Al-Baqara: 165).

**6: Kufuata kunako pingana na kuacha.**
Maana yake: Nikumuabudu Allah pekeyake na kufuata sheria zake, na kuziamini, na kuitakidi ya kwamba ni haki.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni kwake). (Az-Zumar: 54).

**7: Kukubali kunako pingana na kurejesha.**
Maana yake: Ukubali neno hili na ukubali yanayo onyesha neno hili kutokana na Ikhlas katika ibada ya Allah, na kuacha ibada isiyo kuwa yake.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Wao walipo kuwa wakiambiwa La ilaha illa 'Llahu Hapana Allah ila Allah tu, wakijivuna* Na wakisema: Hivyo sisi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu?). (Swafat: 35-36).

**8: Kukanusha vinavyo abudiwa kinyume na Allah.**
Maana yake: Kujitenga na ibada zote zisizokua za Allah, na kuitakidi ya kwamba nibatili.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Allah bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti). (Al-Baqara: 256).

## KUSHAHIDILIA YA KWAMBA MUHAMMAD (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), NI MTUME WA ALLAH

***Dalili yake:** Kauliyake Allah Mtukufu:
(Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma). (At-Tawba: 128).
Na kauli yake Allah Mtukufu: (Na Allah anajua kuwa wewe ni Mtume wa Allah). (Al-Munafiquun: 1).

***Maana yake:**
Kusadikisha moja kwa moja kutoka ndani ya moyo kunako fungamana na kauli ya ulimi ya kwamba Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
ni Mja wa Allah na Mtume wake kwa viumbe woote; Binadamu na Majini.

***Nguzo zake:** Nguzo mbili:
1: Kukiri Utume wake (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Muhammad ni Mtume wa Allah). (Al-Fatihi: 29).
2: Kuitakidi ya kwamba Yeye (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mja wa Allah.
Na dalili: Hakika Allah amemsifu mahala patakasifu kama yeye ni mja, katika sehemu hizo nisehemu za kulingania,
Amesema Allah Mtukufu: (Na hakika Mja wa Allah alipo simama kumwomba, wao walikuwa karibu kumzonga!).
(Al-Jinn: 19). Yeye ni Mtume asiye kadhibishwa, na Mja asiyo abudiwa.

***Masharti yake na viambatanisho vyake:**
1: Kumsadikisha kwake kwa yale aliyo yaeleza.
2: Kumtii kwake kwa yale aliyo amrisha.
3: Na kujiepusha kwa yale aliyo yakataza na kuyakemea.
4: Na asiabudiwe Allah isipokuwa kwa yale aliyo amrisha.

## SHIRKI MAANA YAKE NA VIGAWANYO VYAKE

***Maana ya Shirki:**
**Kilugha:** Inamaana ya ushirikina na kuowanisha.
**Kisheria:** Kumlinganisha asie kua Allah na Allah katika mambo yanayo muhusu Allah.

**Vigawanyo vya shirki:**
**1: Shirki kubwa:**
Ni kila ushirikina ulio tajwa na sheria, na ikawa imekusanya mambo ya kumtoa binadamu katika Uislamu.

**2: Shirki ndogo:**
Ni kila kauli au kitendo kilicho thibiti kisheria kutajwa jina shirki au ukafiri juu yake, na ikajulikana kutokana na dalili za kisheria ya kwamba mwenye kusema au kutenda hayo hatoki katika dini.

***Tofauti kati ya shirki kubwa na shirki ndogo:**
Itaeleweka kupitia jaduwali lifuatalo:

| SHIRKI KUBWA | SHIRKI NDOGO |
|---|---|
| Inamtoa Mtu katika Uislamu | Haimtowi Mtu katika Uislamu |
| Inamuweka milele muhusika ndani ya Moto | Haimuweki muhusika milele ikiwa ataingia |
| Huharibu matendo yote | Hai haribu matendo yote, isipokuwa inaharibu matendo yalio changanyika na Riaa tu |
| Ni halali damu yake na mali yake | Sio halali damu yake na mali yake |

## NAMNA ZA SHIRKI KUBWA

***Shirki kubwa ni namna nne:**
**1: Shirki katika kuomba:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Allah kwa kumsafia ut'iifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha). (Al-Ankabut: 65).

**2: Shirki ya Nia na Makusudio na Kutaka:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Wanao taka maisha ya dunia na pumbao lake tutawalipa humo vitendo vyao kaamili. Na wao humo hawatopunjwa* Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyo yafanya, na yatapotea bure waliyo kuwa wakiyatenda). (Hud: 15-16).

**3: Shirki katika Kutii:**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Allah, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipo kuwa wamuabudu Allah Mmoja, hapana Allah ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo) (At-Tawba: 31).

Na tafsiri yake ambayo haina shaka ndani yake:
Kuwatii wanachuoni na wafanya ibada katika maasi, sio kuwaomba wao, kama alivyo tafsiri Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kumwambia Adiy bin Hatim (Radhi za Allah ziwe juu yake), pindi alipo muuliza akasema: Hatuwaabudu!.
Akamtajia ya kwamba hakika kuwaabudu kwao ni kuwatii katika maasi. Hadithi kaipokea Imam Tirmidhi namba: (3094).

**4: Shirki katika Mapenzi:**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Allah. Wanawapenda kama kumpenda Allah).
(Al-Baqara: 165).

## MIFANO YA SHIRKI KUBWA NA NDOGO

***Mifano kuhusu Shirki kubwa:**
**1: Shirki kubwa iliyo ya wazi:**
Kuchinja kwa asie kua Allah, kuweka nadhiri kwa asie kua Allah, kutaka msaada kwa asie kua Allah.

**2: Shirki kubwa ilio jificha:**
Mfano wa ushirikina wa wanaafiki na ria zao (kujionyesha kwao), na mfano wa khofu ya siri, nayo ni khofu isiokuwa ya Allah katika mambo yasiyo wezekana na yeyote zaidi ya Allah.

***Mifano kuhusu Shirki ndogo:**
1: Shirki ndogo iliyo ya wazi:
Kuapa kwa asiyekuwa Allah, kusema: Akitaka Allah na wewe, na kusema: Bila ya Allah na wewe.
2: Shirki ndogo iliyojificha:
Ria ndogo (kujionyesha), na kuto jituhumu mikosi kwa kurusha ndege.

***Dua yenye manufaa kwa kujilinda na ushirikina:**

Kutoka kwa Abiy Mussa (Radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: Alituhutubia Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), siku moja akasema:
(Enyi watu; Iogopeni shirki hii kwa sababu imejificha sana kuliko mdudu chungu) akawaambia mambo aliyo yataka Allah awambie,

Na vipi tutajikinga nayo niyenye kujificha kama mdudu chungu ewe Mtume wa Allah?
Akasema: (Semeni: Ewe Allah hakika sisi tuna jilinda kwako na kuto kukushirikisha na chochote tunacho kijua, na tuna kuomba msamaha kwa yale tusio ya jua).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Sheikh Albani kasema ni hadithi nzuri- Allah awarehemu wote wa wili.

## HISTORIA YA USHIRIKINA

***Tauhidi ndio asili kwa wanadamu, na ushirikina nijambo lililo zuka na kuingia.**
Kama alivyo sema Ibn Abbas (Radhi za Allah ziwe juu yake): (Baina ya Nabii A'dam na Nabii Nuuh palipita karne kumi woote walikua katika Tauhidi).

***Mwanzo wakutokea ushirikina katika ardhi:**
Katika zama za Nabii Nuuh (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), walipochupa mipaka kwa wema wao,wakatengeneza masanamu yao, kisha ikapelekea jambo hilo kuwaabudu kwao kinyume na Allah, akawatumia Allah Nabii Nuuh (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), awalinganie kwenye Tauhidi.

***Ushirikina kwa watu wa Nabii Mussa (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):**
Imetokea shirki wakati walipo mfanya Ndama kua Allah!.

***Ushirikina kwa Wakristo:**
Umetokea ushirikina baada ya Nabii Issa (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kunyanyuliwa mbinguni, akaja (Paulo) ambae alikuwa akidhihirisha imani ya kumpenda Nabii Issa (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kwa vitimbi na udanganyifu, akaingiza katika dini ya ukristo utatu mtakatifu, na kuabudu msalaba, na mengi katika ushirikina.

***Ushirikina kwa Waarabu:**
Umetokea kupitia mtu mmoja anaitwa: Amru bin Luhai Al-Khuzaiy ambae kabadilisha dini ya Nabii Ibrahim (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), akaleta masanamu katika ardhi ya Hijazi na akaamrisha yaabudiwe.

***Ushirikina katika Ummat Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):**
Umetokea ushirikina kupitia Mashia maarufu Al-Faatwimiyiin baada ya karne ya nne, walipoanza kujengea makaburi, wakazusha bid'a ya maulidi katika Uislamu, na kuchupa mipaka kwa watu wema.
Vilevile imetokea wakati walipo dhihiri masuufiyya wafanyao ibada zisizo sahihi na kuchupa mipaka kwa mashekhe na watu wa muridi.

## HATARI YA USHIRIKINA NA ADHABU ZAKE

**1: Hakika Allah hamsamehe atakapo kufa mshirikina iwapo hakutubia:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Hakika Allah hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye). (An-Nisaa: 48).

**2: Mshirikina ni mwenye kutoka katika Uislamu, ni halali damu yake na mali yake:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na ikisha miezi mitukufu basi wauweni washirikina popote mwakutapo, na washikeni na wazungukeni). (At-Tawba: 5).

**3: hakika Allah hakubali matendo ya mshirikina, na matendo alio yafanya kipindi cha nyuma yatakua ni vumbi tupu:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na tutayaendea yale waliyo yatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi yaliyo tawanyika). (Al-Furqaan: 23).
Na kauli yake: (Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Allah a'mali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri).
(Az-Zumar: 65).

**4: Kwa hakika ni haramu juu yake kuingia peponi, ataishi motoni milele:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Kwani anaye mshirikisha Allah, hakika Allah hawatakuwa na wa kuwanusuru). (Al-Maaida: 72).

## VITENGUZI VYA UISLAMU

Makusudio hapa: vinavyo haribu na kutenganisha na vyo ni vingi, lakini vilivyo hatari zaidi na vinavyo tokea sana ni kumi:

**1:** Kufanya shirki katika ibada ya Allah:
Na miongoni mwa shirki ni kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah, kama yule anaechinja kwa ajili ya jinni au kaburi.
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Hakika Allah hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakae). (An-Nisaa: 116).

**2:** Yeyote atakae jaalia baina yake na Allah -kitu chochote- katikati anawaomba -kuviomba- na ana viomba uombezi na kuvitegemea vitu hivyo (katika mambo ambayo ana yaweza Allah pekeake) amekufuru kwa makubaliano ya wana zuoni.

**3:** Ambae hato wakufurisha washirikina au akawa na shaka katika ukafiri wao au akasahihisha madhehebu yao amekufuru.

**4:** Atakae amini ya kwamba muongozo usio kua wa Mtume Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), umekamilika kuliko muongozo wake, au ya kwamba hukumu ya mwengine nibora kuliko hukumu yake, kama wale ambao wana fa**dhi**lisha hukumu za makafiri dhidi ya hukumu yake huyo ni kafiri.

**5:** Yeyote ambae atachukia kitu chochote alicho kujanacho Mtume Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), hata kama akikifanyia kazi amekufuru.

**6:** Yeyote atakae fanya istihzaa -kejeli dharau- kwa lolote au chochote katika dini ya Allah au katika mambo ya malipo au adhabu amekufuru.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Allah na Ishara zake na Mtume wake?* Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!). (At-Tawba: 65-66).

**7:** Uchawi.
Na miongoni mwa aina za uchawi; kuchukia kitu ulichokua wakipenda, au kupenda kitu ulicho kua wakichukia, kwa njia za uchawi,
Yeyote atakae fanya au kuridhia kwa hilo kakufuru.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru). (Al-Baqara: 102).
**8:** Kuwasaidia washirikina na kuwaunga mkono dhidi ya waislamu.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Allah hawaongoi watu wenye kudhulumu).
(Al-Maaida: 51).

**9:** Atakae amini ya kwamba baadhi ya watu wanayo nafasi ya kutoka katika sheria ya Mtume Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kama alivyo pata nafasi Hidhri kutoka katika sheria ya Nabii Mussa (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), huyo ni kafiri.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri). (Al-Imran: 85).

**10:** Kujitenga mbali na dini ya Allah hajifundishi dini hiyo wala hafanyi yanayo takiwa katika dini.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye kumbushwa kwa Ishara za Mola wake, kisha akazikataa? Hakika Sisi tutajilipiza kwa wakosefu). (As-Sajdah: 22).

**Zinduo 2:**
**1:** Hakuna tofauti kati ya vitenguzi hivi kwa yule anae leta mchezo au mzaha au khofu isipokua kwa yule atakae lazimishwa.
**2:** Vitenguzi hivi vyote ni katika mambo ya hatari, na ni katika mambo yanayo tokea sana, ni lazima kwa Muislamu atahadhari nayo, na aiogopeshe nafsi yake mambo hayo.

## KUMKUFURU TWA'GHUTI

***Maana ya twa'ghuti:**
**Kilugha:** kutokana na Kuchupa mipaka.
**Kisheria:** Ni yale anayo yachupia mipaka mja kwa kinacho abudiwa, au kufuatwa, au kutiiwa.

***Ulazima wa kumkufuru twa'ghuti:**
Jambo la kwanza kulifaradhisha Allah kwa wanadamu ni kumkufuru twa'ghuti na kumuamini Allah.
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allah, na muepukeni Shetani). (An-Nahl: 36).

***Na mna ya kumkufuru twa'ghuti:**
1: Kuitakidi ibada zote kinyume na Allah ni batili, na kuziacha, na uzichukie.
2: Uwakufurishe watu wake na uwachukie.

***Viongozi waki twa'ghuti:**
Ma twa'ghuti ni wengi lakini viongozi wao ni watano:
1: Ibilisi, Allah amlani.
2: Na yeyote anae abudiwa kinyume na Allah akiwa radhi.
3: Yeyote atakae waita watu wamuabudu.
4: Yeyote atakae dai chochote katika mambo ya ghaibu.
5: Na yeyote atakae hukumu kinyume na alivyo teremsha Allah.

## MISINGI MI TATU

1: Mja kumjua Mola wake.
2: Mja Kuijua dini yake.
3: Mja kumjua Mtume wake Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).

**Nayo ndio maswali ya kaburini.**

**Msingi wa kwanza: Mja kumjua Mola wake:**

Ndani yake kuna mas'ala:
1: Hakika Mola wetu ni Allah ambae ametulea na akalea walimwengu wote kwa neema zake.
2: Hakika Allah Mtukufu Yeye ndie Mwenye kuabudiwa, na hatuna sisi mwenye kuabudiwa kinyume naye.
3: Tumemjua Mola wetu kwa alama zake na viumbe vyake vikubwa.
Miongoni mwa alama zake: Usiku na Mchana na Jua na Mwezi.
Na miongoni mwa viumbe vyake: Mbingu saba na Ardhi saba na vilivyomo ndani yake na baina yake.

**Msingi wa pili: Mja Kuijua dini yake:**

Ndani yake kuna mas'ala:
1: Dini ambayo hatokubali Allah dini nyingine tofauti na Uislamu.
2: Uislamu ni: kujisalimisha kwa Allah kwa Tauhidi, na kufuata kwa kutii, na kujiepusha na ushirikina na watu wake.

**3: Daraja za Dini ni tatu:**

1: Uislamu.
2: Imani.
3: Ihsani.

**Msingi wa tatu: 3: Mja kumjua Mtume wake Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):**

Ndani yake kuna mas'ala:

**1: Jina lake na nasabu yake:**

Yeye ni Muhammad bin Abdillahi bin Abdil-mutwalib bin Haashim, na Haashim kutokana na Quraishi, na Quraishi kutokana na waarabu, na waarabu ni katika kizazi cha Nabii Ismail bin Ibrahim Kipenzi cha Allah.

**2: Umri wake:**

Anaumri wa myaka (63), myaka (40) kabla ya kupewa utume, na myaka (23) baada ya kuwa Nabii.

**3: Utume wake na ujumbe wake:**

Kapewa Unabii kwa Iqra'a, na kapewa Utume kwa Mudathir.

**4: Mji wake na alipo hamia:**

Mji wake: Makkah.
Na akahamia Madina.

**5: Madhumuni ya Daawa yake:**
Ametumwa na Allah kuwaonya kutokana na ushirikina, na alinganie katika Tauhidi.

## UKAFIRI

***Maana yake:**
**Kilugha:** Ina maana ya kusitiri na kufunika.
**Kisheria:** Kinyume na Uislamu.

***Namna zake:**
1: Ukafiri mkubwa.
2: Ukafiri mdogo.

***Ukafiri mkubwa:**
Ndani yake kuna mas'ala:
1: Maana yake:
Ni kuto muamini Allah na Mitume wake, sawasawa umewapinga au hukuwapinga.

**2: Hukumu yake:**
Inamtoa muhusika kwenye dini.

**3: Namna zake** Ni tano:
**1: Ukafiri wa kukadhibisha:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzulia uwongo Allah au anaye kanusha Haki inapo mjia? Je! Si katika Jahannamu ndio yatakuwa makaazi ya makafiri?). (Al-Ankabut: 68).

**2: Ukafiri wa kukataa na kufanya kibri pamoja na kukubali:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia wote isipo kuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika makafiri). (Al-Baqara: 34).

**3: Ukafiri wa shaka- nao ni ukafiri wa dhana:**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na akaingia katika bustani yake, naye hali anajidhulumu nafsi yake. Akasema: Sidhani kabisa kuwa haya yataharibika* Wala sidhani kuwa hiyo Saa (ya Kiyama) itatokea. Na ikiwa nitarudishwa kwa Mola wangu Mlezi, bila ya shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya* Mwenzake akamwambia kwa kubishana naye: Je! Unamkufuru aliye kuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha akakufanya mtu kaamili?* Lakini Yeye Allah ndiye Mola wangu Mlezi. Wala simshirikishi na yeyote). (Al-Kahf: 35-38).

**4: Ukafiri wa kujiepusha:**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Na walio kufuru wanayapuuza yale wanayo onywa). (Al-Ahqaaf: 3).

**5: Ukafiri wa unaafiki:**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote). (Al-Munafiquun: 3).

***Ukafiri mdogo:**
Ndani yake kuna mas'ala:

**1: Maana yake:**
Kila maasi yalio tajwa ndani ya Qur'ani na Sunna kama ni ukafiri na haukufikia kwenye kilele cha ukafiri mkubwa.

**2: Hukumu yake:**
Ni haramu, na nikatika madhambi makubwa, lakini muhusika hatoki katika Uislamu.

**3: Mifano yake:**
1: Kukufuru neema, Amesema Allah Mtukufu:
(Lakini ukazikufuru neema za Allah). (An-Nahl: 112).
2: Muislamu kupigana na ndugu yake Muislamu.
(Kumtukana Muislamu ni uovu, na kupigana nae ni ukafiri).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.
3: Kutoa kejeli kwenye nasabu za wengine.
4: Kuomboleza wakati wa msiba: (Mambo mawili kwa watu ni ukafiri: kutoa kejeli kwenye nasabu, na kuomboleza wakati wa msiba).
Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

## UNAAFIKI

***Maana yake:**
**Kilugha:** Kufich kitu na kufunika.

**Kisheria:** Kudhihirisha Uislamu na kuuficha ukafiri na shari.

***Maana za unaafiki:**
Ni namna mbili:
1: Unaafiqi mkubwa wa kiitikadi.
2: Unaafiqi mdogo wa kimatendo.

Nijuu yako kufafanuliwa:
***Unaafiki wa kiitikadi:**
Ndani yake kuna mas'ala:
**1: Maana yake:**
Nao ni unaafiki mkubwa ambao muhusika hudhihirisha Uislamu na kuficha ukafiri.

**2: Hukumu yake:**
Humtoa mtu katika Uislamu moja kwa moja, na muhusika atakua katika daraja ya chini kabisa ya moto wa jahannam.

**3: Namna zake:**
Ni namna sita:
1: Kumkadhibisha Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
2: Kukadhibisha baadhi ya alio kujanayo Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
3: Kumchukia Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
4: Kuchukia baadhi ya alio kujanayo Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
5: Kufurahi kwa kushuka Uislamu wa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
6: Kuchukia kwa kupata nusra dini ya Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).

***Unaafiki wa kimatendo:**
Ndani yake kuna mas'ala:
**1: Maana yake:**
Nikufanya jambo katika matendo ya wanaafiki pamoja na kubakia Imani ndani ya moyo.

**2: Hukumu yake:**
Haimtowi mtu katika Uislamu, lakini jambo hilo ni haramu na nikatika madhambi makubwa, muhusika anakuwepo na imani na unaafiqi, na unapo zidi husababisha kuwa mnaafiqi wa moja kwa moja.

**3: Mifano yake:**
1: Uongo katika mazungumzo: (Anapo zungumnza hudanganya).

2: Kukhalifu ahadi: (Na anapo ahidi hutimizi).
3: Kukhini amana: (Na anapo aminiwa hufanya khiyana).
4: Uovu katika ugonvi: (Na anapo gombana hufanya uovu).
5: Udanganyifu katika mikataba: (Na anapo weka mkataba hutapeli).
6: Kuona uvivu kwenda kuswali Jamaa muskitini:
(Na wanapo inuka kusali huinuka kwa unyong'onyo). (An-Nisaa: 142).
7: Kujionyesha katika matendo mema:
(Wanajionyesha kwa watu tu). (An-Nisaa: 142).

## AL-WALAA WAL-BARAA (KUPENDA NA KUCHUKIA KWA AJILI YA ALLAH)

***Maana yake Kilugha:**
Al-walaa: Ni kutokana na wilaya nalo ni mapenzi.
Al-Baraa ki lugha:
Nichimbuko la neno barii kwa maana ya kukata.

***Kisheria:**
Al-walaa: Kuwapenda Waisilamu na kuwanausuru na kuwakirimu na kuwaheshimu na kuwa karibu nao.
Al-baraa: Kuwachukia makafiri na kuwa mbali nao na kuacha kuwanusuru.

***Umuhimu wa Al-walaa na Al-baraa:**
1: Ni katika misingi ya itikadi ya Uislamu.
2: Ni kamba madhubuti ya Imani.
3: Hakika ndio mila ya Nabii Ibrahim na Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).

***Vigawanyo vyo kupenda:**
Namna mbili:
1: Kuwafanya vipenzi vya ndani.
2: Kuwapenda.

***K uwafanya vipenzi vya ndani:**
Ndani yake kuna mas'ala:

**1: Maana yake:**
-Kuupenda ushirikina na washirikina, na kuupenda ukafiri na makafiri.
-Kuwanusuru makafiri dhidi ya Waislamu.

**2: Hukumu yake:**
Ni ukafiri mkubwa na kutoka katika Uislamu.

**3: Dalili:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao). (Al-Maaida: 51).

***Kuwapenda:**
Ndani yake kuna mas'ala:

**1: Maana yake na udhibiti wake:**
Kuwapenda makafiri na washirikina kwa sababu ya dunia, hakuna ndani yake kuwanusuru, la sivyo itakuwa ni kuwapenda mapenzi ya ndani.

**2: Hukumu yake:**
Ni haramu na ni katika madhambi makubwa.

**3: Dalili:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi).
(Mumtahinah: 1).

***Namna za kuwapenda makafiri:**
Miongoni mwazo:
1: Kujifananisha nao katika mavazi na maneno.
2: kusafiri kwenda katika miji yao kwa lengo la matembezi au kuiburudisha nafsi.
3: Kuishi katika miji yao na kuto kuhama kuelekea katika miji ya Waislamu kwa lengo la kuikimbia dini.
4: Kujipamba na historia zao kama historia za kucheza kwao na sikukuu zao za kuzaliwa.
5: Kushirikiana nao katika sikukuu zao au kuwasaidia katika kuzisimamisha au kuwapongeza katika minasaba yao au kuhudhuria sehemu hizo.
6: Kujiita majina yao.

## VIGAWANYO VYA WATU KWA YANAYO FAA KATIKA HAKI ZAO KWA KUWAPENDA NA KUWACHUKIA

Watu katika kuwapenda na kuwachukia wamegawanyika sehemu tatu:
1: Kuna wanao pendwa mapenzi ya kweli kabisa hakuna uaduwi ndani yake.
Nao ni Waumini walio safi kabisa.
2: Kuna wanao chukiwa na kuwafanyia uaduwi pasipokuwa na mapenzi ndani yake wala kuwanao karibu.
Nao ni Makafiri barabara.
3: Kuna wanao pendwa kwa namna Fulani na kuchukiwa kwa namna nyingine.
Nao ni wafanya maasi katika Waumini, hupendwa kwa kuwa kwao na Imani, na huchukiwa kwa kuwa kwao na maasi ambayo yapo chini ya ukafiri na ushirikina.

## UISLAMU

***Uislamu Ki Lugha:**
Ni kufuata na kujisalimisha na unyenyekevu.

***Uislamu Ki Sheria: Ni:**
1: Kujisalimisha kwa Allah kwa kumpwekesha.
2: Na kumfuata yaye kwa kutii.
3: Na kujitenga mbali na ushirikina na washirikina.

***Uislamu kwa maana ya ujumla na maana finyu:**
1: Uislamu kwa maana ya ujumla:
Ni kumuabudu Allah kwa yale alio amrisha tokea aanze kutuma Mitume hadi kusimama kiyama.
2: Uislamu kwa maana finyu:
Unahusiana nayale aliyo tumwa nayo Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).

## NGUZO ZA UILSAMU

***Ni tano:**
1: Kushahidilia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu, na Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mtume wake.
2: Kusimamisha Swala.
3: Kutoa Zaka.
4: Kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani.
5: Kwenda kuhiji nyumba tukufu kwa mwenye uwezo njia ipo.

*Nazo zimegawanyika katika sehemu mbili:
**1: Nguzo ambazo halisimami jengo isipokuwa kwa nguzo hizo, huitwa (Nguzo za msingi).**
Nazo ni nguzo mbili:
1: Shahada mbili.
2: Kusimamisha Swala.

**2: Nguzo ambazo halikamiliki jingo isipokuwa kwa nguzo hizo, huitwa (Nguzo za kukamilisha).**
Nazo ni tatu:
1: Kutoa Zaka.
2: Kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani.
3: Kwenda Hijja.

***Dalili ya nguzo za Uislamu:**
Kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushahidilia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mmoja tu, na Muhammad

(Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mtume wa Allah, na Kusimamisha Swala, na Kutoa Zaka, na Kuhijji nyumba tukufu, na Kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

## IMANI

***Maana yake upande wa Lugha:**
Kusadikisha na kukiri.

***Imani upande wa Ahlu-sunna wal-jamaa:**
**Ni:**
1: Kuitakidi Moyoni.
2: Na Kutamka kwa ulimi.
3: Na Kufanya kazi vitendo.
4: Inazidi kwa kufanya mema.
5: Na Inapunguwa kwa kufanya maasi.

## NGUZO ZA IMANI

***Ni sita:**
1: Kumuamini Allah.
2: Na Malaika wake.
3: Na Vitabu vyake.
4: Na Mitume wake.
5: Na Siku ya mwisho.
6: Na Qadari (makadara) kheri na shari.

Nijuu yako kufahamu yanayo fungamana na kila nguzo:
**1: Kumuamini Allah:**
Inafungamana na mambo ma nne:
1: Kuamini kuwepo Allah.
2: Kuamini ya kwamba Allah ndie muendeshaji wa mambo.
3: Kuamini ya kwamba Allah ndiye anae stahiki Ibada.
4: Kuamini majina yake na sifa zake.

**2: Kuwaamini Malaika:**
Inafungamana na mambo ma nne:
1: Kuamini kuwepo kwao.
2: Kuamini wale tunao fahamu majina yao kama: Jibril (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na wale tusio wajua majina yao tuna waamini kwa ujumla.
3: Kuamini yale tunayo yajuwa kutokana na sifa zao.
4: Kuamini wale tunao wajuwa kutokana na kazi zao wanazo zifanya kwa Amri ya Allah.

**3: Kuamini Vitabu:**

Inafungamana na mambo manne:

1: Kuamini ya kwamba ni kweli vimeshuka kutoka kwa Allah.

2: Kuamini tunavyo vijua majina yake kama: Qur'ani na Taurati na Injil.

3: Kusadikisha yalio thibiti kutokana na habari zake kama Qur'ani na habari za vitabu vilivyo tangulia ikiwa havija badilishwa au kugeuzwa kwa yale yalio nukuliwa kwa usahihi katika sheria yetu.

4: Kufanyiwa kazi hukumu zilizomo ikiwa hazijafutwa, na kuridhika na kusalim amri sawasawa tukifahamu hekima yake au hatukufahamu, na vitabu vyote vilivyo tangulia vimefutwa na Qur'ani.

**4: Kuamini Mitume:**

Inafungamana na mambo ma nne:

1: Kuamini ya kwamba Ujumbe wao ni wakweli kutoka kwa Allah Mtukufu, Yeyote atakae kufuru ujumbe wa Mtume Mmoja miongoni mwao; kwa hakika kawakufuru wote.

2: Kuamini wale tunao wafahamu majina yao, mfano: Muhammad na Ibrahim na Mussa na Issa na Nuuh (a.s).

3: Kusadikisha yalio sahihi katika habari zao.

4: Kuzifanyia kazi sheria za yule alie tumwa kwetu miongoni mwao naye ni Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na Yeye ndie wa mwisho wao na alie tumwa kwa watu wote.

**5: Kuamini siku ya mwisho:**

Inafungamana na mambo ma tatu:

1: Kuamini kufufuliwa.

2: Kuamini kuhesabiwa na kulipwa.

3: Kuamini Pepo na Moto.

Na inaingia katika Imani ya siku ya mwisho: Kuamini kila kitacho tokea baada ya kufa, ikiwemo misukosuko ya kaburini na adhabu zake na neema zake.

**6: Kuamini Qadari (makadara):**

Inafungamana na mambo ma nne:

1: Kuamini ya kwamba Allah Mtukufu anafahamu kila kitu kwaujumla na ufafanuzi.

2: Kuamini ya kwamba hakika Allah kaandika yote katika Ubao ulio hifadhiwa.

3: Kuamini ya kwamba vitu vyote havitokei isipokuwa kwa matashi ya Allah Mtukufu.

4: Kuamini ya kwamba vitu vyote ni viumbe vya Allah Mtukufu, uhalisia wake na sifa zake na haraka zake.

***Dalili juu ya nguzo sita za Imani:**
1: Amesema Allah Mtukufu: (Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Allah na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii). (Al-Baqara: 177).
2: Kauli yake Allah Mtukufu:
(Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo). (Al-Qamar: 49).
3: Na katika sunna imepokelewa katika hadithi ya Jibril (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), wakati alipo muuliza Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na akasema: nieleze kunako Imani? Akasema: (Ni kumuamini Allah na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho na kuamini qadari kheri yake na shari yake). Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

## IH'SANI (wema)

***Maana yake:**
**Kilugha:** Ni kinyume na ubaya.
**Kisheria:** Ni kujichunga kwaajili ya Allah kwa siri na dhahiri.

***Nguzo za Ihsani:**
Nguzo moja:
Nayo ni: (Kumuabudu Allah kana kwamba unamuona, ikiwa humuoni hakika Yeye anakuona).

***Vigawanyo vya Ihsani:**
Vigawanyo namna mbili:
1: Ihsani kwa viumbe:
Inakuwa katika mambo ma nne:
1: Mali.
2: Cheo.
3: Elimu.
4: Mwili.

**2: Ihsani katika Ibada ya Muumbaji:**
Hili lina daraja mbili:
1: Daraja ya kushuhudia: (Unamuabudu Allah kanakwamba unamuona), nayo ndio daraja ya juu kati ya daraja mbili.
2: Daraja ya kuangalia na kuchunga:
(Ikiwa Wewe humuoni fahamu ya kwamba Yeye anakuona).

***Dalili kuhusu Ihsani:**
1: Kauli yake Allah Mtukufu: (Hakika Allah yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema). (An-Nahl: 128).
2: Kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), wakati alipo ulizwa na Jibril (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), kuhusu Ihsani: (Una muabudu Allah kanakwamba unamuona, ikiwa humuoni hakika Yeye anakuona).
Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

## MAHUSIANO KATI YA UISLAMU NA IMANI NA IHSANI

**1: Vitakapo tajwa vitu hivi vi tatu sehemu moja kila kimoja kina maana maalumu:**
1: Hukusudiwa Uislamu; Matendo ya nje.
2: Hukusudiwa Imani; Mambo ya ghaibu (yasiyo onekana).
3: Na Hukusudiwa Ihsani; Daraja ya juu kabisa ya dini.

**2: Mambo haya ma tatu yatakapokuwa tofauti tofauti:**
1: Utakapokuwa Uislamu pekeyake; Imani huingia ndani.
2: Itakapokuwa Imani pekeyake; Uislamu huingia ndani.
3: Itakapokuwa Ihsani pekeyake; huingia Uislamu na Imani.

## IBADA

***Maana yake:**
**Kilugha:** Kujidhalilisha na unyenyekevu.
**Kisheria:** Ni jina linalo kusanya kila anacho kipenda Allah na kukiridhia, kutokana na maneno na vitendo vya ndani na nje.

***Sababu ya kuitwa kazi za kisheria kwa walio lazimishwa na sheria kuwa Ibada:**
Kwa sababu wao wanatekeleza na kufanya haliyakuwa ni wanyenyekevu wenye kudhalilika kwaajili ya Allah.

***Nguzo za Ibada:**
Ni tatu:
1: Mapenzi.
2: Khofu.
3: Kutaraji.

***Sharti za kusihi Ibadan na kukubaliwa kwake:**
Sharti mbili:
**1: Ikhlas (kutakasa).**
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:
**(Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allah kwa kumtakasia Dini**). (Al-Bayyinah: 5).
**2: Kumfuata Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).**

Na dalili kauli yake (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae fanya amali hakuna ndani yake amri yetu jambo hilo nilenye kurejeshwa).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

***Ibada zipo namna mbili:**
1: Ibada za Ulimwenguni.
2: Ibada za Kisheria.

***Ibada za Ulimwenguni:**
Maana yake: nako ni kunyenyekea kwa Amri za Allah za kidunia.
Nayo hukusanya viumbe vyote hatoki hata mmoja: Muumini, na Kafiri, na Mwema, na Muovu.
Dalili yake kauliyake Allah Mtukufu: (Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa wake). (Maryam: 93).

***Ibada za Kisheria.**
Maana yake: nako ni Kunyenyekea kwa amri za Allah Mtukufu za kisheria.
Nazo ni maalum kwa wenye kumtii Allah na kufuata waliyo kujanayo Mitume.
Dalili yake kauliyake Allah Mtukufu:
(Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha). (Al-Furqaan: 63).

## KANUNI MUHIMU KATIKA TAUHIDI YA IBADA

***kipengele cha kanuni:**
(Kitendo chochote ambacho ni Ibada, kukipeleka kwa Allah ni Tauhidi, na kukipeleka kwa asie kuwa Allah ni shirki na kushirikisha).

***Dalili ya kanuni hii:**
Dalili ni nyingi miongoni mwazo:
Kauli yake Allah Mtukufu: (Muabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote). (An-Nisaa: 36).
Na kauli yake Allah Mtukufu: (Na Mola wako ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu). (Al-Israai: 23).
Na kauli yake Allah Mtukufu:
(Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote). (Al-An'aam: 151).

***Mifano:** Dua ni Ibada, kuipeleka kwa asie kuwa Allah ni ushirikina.
Khofu ni Ibada, kutumia kwa asie kuwa Allah ni ushirikina.
Kuchinja ni Ibada, kufanya kwa asie kuwa Allah ni ushirikina.
Nadhiri ni Ibada, kuitumia kwa asie kuwa Allah ni ushirikina.

## VIGAWANYO VYA MAPENZI

Yamegawanyika mapenzi katika sehemu nne:

**1: Ibada:**

*Nayo ni kumpenda Allah.

*Na kupenda anavyo vipenda Allah.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Lakini walio amini wanampenda Allah zaidi sana). (Al-Baqara: 165).

**2: Shirki:**

Nayo ni kupenda asiye kuwa Allah pakiwemo kudhalilika na kumtukuza huyo anae pendwa kwa yale yasio faa isipokuwa kwa Allah tu.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Allah. Wanawapenda kama kumpenda Allah). (Al-Baqara: 165).

**3: Maasi:**

Nayo ni kama kupenda maasi na bid'a na mambo ya haramu.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Allah anajua na nyinyi hamjui). (An-Nuur: 19).

**4: Mapenzi ya kawaida:**

Kamavile kuwapenda watoto na mke na nafsi na mengineyo nayo hufaa.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, na wana, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Allah ndio kwenye marejeo mema).
(Al-Imran: 14).

## KHOFU (kuokopa)

***Maana yake:** (Ni jambo linalo jitokeza hupatikana ndani yake yanayo pelekea kuangamia au madhara au udhia).

***Namna za khofu:**

**1: Shirki kubwa:**

Nayo ni khofu ya siri: Ni kumukhofu asie kuwa Allah kwa yale asio ya weza zaidi ya Allah.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini). (Al-'Imran: 175).

**2: Ya haramu:**

Nayo ima kuacha yaliyo wajibu au kufanya yalio haramu kwaajili ya kuwakhofu watu.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:

(Basi msiwaogope watu, bali niogopeni Mimi). (Al-Maaida: 44).

**3: Inayo faa:**

Nayo ni khofu ya kawaida, kama khofu ya kuokopa simba na adui na kiongozi muovu na mfano wahao.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu:

(Akapambazukiwa mjini asubuhi naye ana khofu, akiangalia huku na huku). (Al-Qasas: 18).

**4: Ibada:**

Nayo ni kumukhofu Allah pekeyake hana mshirika.

Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi atapata Bustani mbili). (Ar-Rahman: 46).

***Namna za kumukhofu Allah:**

Namna mbili:

1: Yenye kusifiwa (khofu).

Nayo niile ambayo inakuzuia baina yako na baina ya kumuasi Allah, inakupeleka katika kufanya yalio wajibu na kuacha yalio haramu.

2: Isiyo sifiwa (khofu).

Nayo niile ambayo inampelekea mja kukata tamaa na Rehma za Allah.

# KUTARAJI

***Maana yake:**
Ina maana ya kuwa na matumaini na tamaa na matarajio na kusubiri kitu kinacho pendwa.

***Vigawanyo vyake:**
Vigawanyo vi tatu:
**1: Kutaraji kwa Ibada:**
Nako ni kumtarajia Allah pekeyake asie kuwa na mshirika, nako kuko namna mbili:

**1: Kutaraji kunako sifiwa:**
Nako ni kutaraji kunako ambatana na matendo yalio mazuri na kumtii Allah.

**2: Kutaraji kunako chukiza:**
Nako ni kutaraji bila ya matendo mema nako ni kujipa moyo na kujidanganya.

**2: Kutaraji kwa ushirikina:**
Nako ni kumtarajia asie kuwa Allah katika mambo asio yamiliki zaidi ya Allah.

**3: Kutaraji kwa kawaida:**
Utakapo tarajia jambo Fulani kwa Mtu analo miliki na anauwezo nalo, kama kusema: (Nataraji uhudhurie).

***Dalili ya kutaraji:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake). (Al-Kahf: 110).

# KUTEGEMEA

***Maana yake:**
**Ki Lugha:** Kuegemeza na kutegemea.
**Ki Sheria:** Nako ni kuutegemeza moyo kwa Allah pekeyake.

***Kutegemea upande wa kisheria:**
Nikule ambako kumekusanya mambo matatu:
1: Kutegemea kwa Allah kutegemea kwa kweli kabisa.
2: Kua na uhakika na Allah na kuitakidi ya kwamba mambo yote yapo mikononi mwake.
3: Kufanya sababu zilizo amrishwa kisheria.

***Vigawanyo vya kutegemea:**
Vigawanyo vitatu:
**1: Kutegemea kwa Ibada:**
Nako ni kutegemea kwa Allah pekeyake hana mshirika.

**2: Kutegemea kwa Ushirikina:**
Kama kutegemea kwa asie kuwa Allah katika mambo yanayo muhusu Allah.
Na kama kutegemea moja kwa moja au kuto kutegemea moja kwa moja juu ya sababu.

**3: Kuwakilisha:**
Nako ni kumuwakilisha mtu afanye kazi kwa niyaba yako kutokana na mambo anayo ya weza, jambo hilo linaruhusiwa.

***Na tofauti kati ya Kutegemea na Kuwakilisha:**
Hakika kutegemea: Ni mambo ya ndani ya moyo.
Na kuwakilisha: Ni mambo ya wazi.

***Dalili ya kutegemea:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Na mtegemeeni Allah ikiwa nyinyi ni Waumini). (Al-Maaida: 23).

## DUA (maombi)

***Dua ni Ibada:**

Dua ni jambo muhimu katika namna za ibada kwa kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Dua ndiyo Ibada). Kapokea hadithi hii Imam Tirmidhi.

Na kauli yake Allah Mtukufu:

(Na hakika misikiti ni ya Allah, basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah). (Al-Jinn: 18).

***Namna za Ibada:**

Namna mbili:

**1: Dua ya Ibada:**

Makusudio yake: Kila matendo ayafanyayo binadamu kwa ajili ya Mola wake.

Mfano wake: Swala, na Hijja, na Sadaka, na Swaumu.

Sababu ya kuitwa (Dua): kwa sababu ndani yake kuna maana ya kutaka, kana kwamba binadamu wakati anapofanya matendo hutafuta kutoka kwa Allah amrehemu kwa matendo hayo na amuingize Peponi.

**2: Dua ya Suala:**

Makusudio yake: maombi ambayo ndani yake kuna kuomba na kutafuta.

Mfano wake: kama kusema:

(Ewe Allah ni hurumie, Bwana nisamehe).

***Dua (kufanya maombi) kwa asie kuwa Allah:**

Dua ni Ibada, Yeyete atakae ipeleka kwa asie kua Allah huyo ni mshirikina tena kafiri.

Na kauli yake Allah Mtukufu: (Na anaye muomba - pamoja na Allah - Allah mwenginewe hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi). (Al-Muuminuun: 117).

## RUQYA (tiba)-(zinguo)

***Maana yake:**
**Kilugha:** Ni wingi wa tiba nako ni kujikinga.
**Kisheria:** Ni aya na adhkari (nyiradi), na dua husomewa mgonjwa.

***Vigawanyo vyake:**
Ni viwili:
1: Ruqya ya kisheria.
2: Ruqya isiyo ya kisheria.

***Ruqya ilio ya kisheria:**
Niile ilio kusanya sharti tatu kwa makubaliano ya wanachuoni:
1: Iwe kwa ulimi wa kiarabu ulio wazi na yenye kufahamika maana yake.
2: Iwe kwa maneno ya Allah au majina yake au sifa zake.
3: Asiitegemee tiba hiyo moja kwa moja, bali aitakidi ya kwamba matibabu hayaathiri yenyewe bali kwa makadara ya Allah.

***Ruqya isiyo ya kisheria:**
Niile ilio pungua sharti moja katika masharti ya ruqya ya kisheria au zaidi ya masharti.

***Dalili katika Sunna kuhusu Ruqya:**
Maneno yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Hakika Ruqya na Hirizi na Dawa za mapenzi ni shirki). Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Abu'Daudi.
Na kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Nionyesheni Ruqya zenu (matibabu yenu), Hakuna tatizo katika Ruqya (matibabu), ambayo ndani yake hakuna shirki). Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

## HIRIZI

***Maana yake:**
**Kilugha:** Ni wingi wa hirizi
**Kisheria**: Ni vinavyo ning'inizwa kwenye shingo za watoto na wengineo kwa lengo la kuondo Kijicho.

***Vigawanyo vyake:**
Ni viwili:

**1: Hirizi za Qur'ani na Nyiradi za Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):**
Na ilio kuwa sahihi ni kuzuia kwa sababu tatu:
1: Ujumla wa katazo kuhusu hirizi na hakuna kinacho baguwa kwenye ujumla huu.
2: Kufunga mlango huo huenda ikawa ni sababu ya kuning'iniza yasiyo kuwa halali.
3: Kwa hakika itapelekea kuto heshimiwa yule alie ning'iniza wakati wa kuingia nayo chooni kwa kukidhi haja.

**2: Hirizi isiokuwa ya Qur'ani wala nyiradi za Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):**
Kama zile ambazo huandikwa majina ya majini na mashaitwani, na huwa ndani yake twalasimu zisizo fahamika, haya ni haramu moja kwa moja, na hayo nikatika ushirikina kwa sababu ndani yake kuna kufungamana na asie kuwa Allah.

***Hitimisho:**
Hakika hirizi zote ni haramu, sawasawa ziwe za Qur'ani au nyingine, na ikiwa tofauti na Qur'ani ni haramu na ni shirki.

Na dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Hakika Ruqya na Hirizi na Dawa za mapenzi ni shirki).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Abu'Daudi.

## KUTAKA BARAKA

***Maana ya kutaka Baraka:**
**Kilugha:** Kuzidisha kitu na kuthibiti kwake.
**Kisheria**: Kutafuta Baraka na kuitarajia na kuiitakidi.

***Vigawanyo vya kutaka Baraka:**
Ni viwili:
1: Kutaka Baraka kuliko ruhusiwa.
2: Kutaka Baraka kusiko ruhusiwa.

***Kutaka Baraka kuliko ruhusiwa:**
1: Kutaka Baraka kwa dhati ya Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na vinavyo patikana kutoka katika mwili wake.
Jambo hili ni maalumu kwa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), katika uhai wake tu.
2: Kutaka Baraka kwa maneno na matendo ya kisheria atakapo yafanya mja hufikiwa na kheri na Baraka.
Kama kusoma Qur'ani, na kumtaja Allah, na kuhudhuria vikao vya elimu.

3: Kutaka Baraka katika sehemu alizo jaalia Allah kuwa na Baraka, kama vile Misikiti na miji mitukufu Makkah na Madina na Sham.
Na makusudio ya kutaka Baraka sehemu hizo: kufanya yalio ya kheri na kumuabudu Allah kwa matendo yalio ya sheria,
Na sio makusudio kujifuta na kuta za msikiti au kujipaka kutoka katika nguzo zake.

4: Kutaka Baraka katika zama alizo jaalia Allah kuwa na ubora na Baraka.
Kama mwezi mtukufu wa Ramadhani, na kumi la mwanzo katika mwezi Mtukufu wa Dhul-hijja, na usiku wa Lailatul-qadri, na Theluthi ya mwisho ya usiku.
Na inakuwa kutaka Baraka katika nyakati hizo: kwa kuzidisha matendo mema na kumuabudu Allah ndani yake kwa matendo ya kisheria.

5: Kutaka Baraka kupitia vyakula alivyo jaalia Allah ndani yake Baraka.
Kama mafuta ya Zaituni, Asali, na Maziwa, na Habbat'sauda, na Maji ya zam zam.

*Maji ya zam zam hayaondoki Baraka zake kwa sababu ya kuondolewa mahala pake kupelekwa mahala pengine, kwa kauli ilio sahihi ya wanachuoni.

***Kutaka Baraka kusiko ruhusiwa:**

1: Kutaka Baraka kusiko ruhusiwa sehemu na kwenye vitu visivyo sema:
Mfano:
*Kujipangusa kwenye kuta za sehemu ambayo imethibiti kisheria kama pana Baraka, na kubusu madirisha yake na nguzo zake na kutaka tiba kwa udongo wake.
*Kutaka Baraka kwenye makaburi ya watu wema.
*Kutaka Baraka sehemu za matukio za kihistoria kama sehemu alipo zaliwa Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), au katika pango la mlima wa Jabali Hira (sehemu wahyi ulipo shuka). Au katika pango la Thaur (sehemu alipo ingia Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na Abubakar (Radhi za Allah ziwe juu yake), wakati wa Hijra (kutoka makkah kuelekea madina)).

**2: Kutaka Baraka kusiko ruhusiwa kwa zama:**

*Kufanya mambo yasio kuwa ya kisheria na Ibada za uzushi katika zama ambazo zimethibiti kisheria kuwa zina Baraka.

***Kutaka Baraka kwa zama ambazo hazikuthibiti kisheria ndani yake Baraka.**

Mfano: (Kuzaliwa kwa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na usiku wa Isra na Miiraj, na usiku wa nusu katika mwezi wa Shaaban, na usiku na mchana ulio tokea tukio la kihistoria).

**3: Kutaka Baraka kusiko ruhusiwa kupitia miili ya wema na athari zao:**

*Haifai kutaka Baraka kwa yeyote miongoni mwa wanadamu isipokuwa kwa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na athari zake, na hili ni maalum katika uhai wake tu.

***Kanuni na vidhibiti muhimu katika kutaka Baraka:**

1: Kutaka Baraka ni Ibada, na asili katika ibada ni kuzuia mpaka paje dalili ya kuruhusu kwake.
2: Kutaka Baraka kote hutoka kwa Allah pekeyake, Yeye ndiye mwenye kuimiliki na mwenye kuitoa, isitafutwe kwa mwengine.
3: Hakika kutaka Baraka kwa vile vilivyo thibiti kama vina Baraka, havileti faida isipokuwa kwa mwenye kumpwekesha Allah mwenye kumuamini Allah na Mtume wake (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
4: Hakika kutaka Baraka kwa vile vilivyo thibiti na vina Baraka kisheria ni lazima iwe katika mfumo wa kisheria na wala wasizue ndani yake namna Fulani na njia ambazo hazikufanywa na wema wa mwanzo.

## KANUNI MUHIMU KATIKA MLANGO WA SABABU

1: Kutegemea sababu ni lazima iwe kwa Allah Mtukufu, na sio kwenye sababu yenyewe, kwa sababu Allah Mtukufu ndie mwenye kuisababisha hiyo sababu na kuwepo kwake.
2: Afahamu ya kwamba hizo sababu ni zenye kuambatana na makadara ya Allah.
3: Njia ya kuthibitisha kwamba jambo Fulani ni sababu ni vitu viwili:

**1: Kwa njia ya kisheria.**
Mfano: Asali ni sababu ya tiba.
Na dalili yake kauli yake Allah Mtukufu:
(Ndani yake kina matibabu kwa wanaadamu). (An-Nahl: 69).

**2: Kwa njia ya kujaribu.**
Mfano: Moto ni sababu ya kuunguwa, lakini hapana budi kupatikana njia ya kujaribu sababu ya kitu Fulani njia ya wazi baada ya kutumia kitu chenyewe moja kwa moja; kwa sababu kuthibitisha kwa njia isiyo ya wazi moja kwa moja hupelekea madai ya kitu Fulani, mfano wa wale wanao vaa bangili kwamba yaondoa Kijicho!.

## TAWASULI

***Maana yake:**

**Kilugha:** Ni kutokana na ukaribu, lakini katika asili: ni kinacho tumiwa kwaajili ya kukuunganisha na kitu kingine na kukukurubisha kwacho.

**Kisheria**: Ni kufanya sababu za kisheria zinazo kukurubisha mbele ya Allah Mtukufu.

***Vigawanyo vyake:**

Ni viwili:

1: Tawasuli Inayo faa.

2: Tawasuli Isiyo faa.

***Tawasuli Inayo faa:**

Zipo namna tatu:

1: Tawasuli kwa kutumia majina ya Allah Mtukufu au sifa miongoni mwa sifa zake.

2: Tawasuli kwa kutumia matendo mema alio yafanya muombaji.

3: Tawasuli kwa kutaka Dua ya mtu mwema alie hai.

***Tawasuli Isiyo faa:**

Nayo ni tawasuli isiyo kusanya mambo matatu yalio tajwa katika tawasuli inayo faa, na miongoni mwa hayo:

1: Kufanya tawasuli kwa Allah Mtukufu kupitia haki au cheo cha mtu.

2: Kufanya dua au nadhiri kwaajili ya mawalii na wema.

3: Kuchinja kwaajili ya roho za mawalii na kukaa kwenye kaburi zao.

## KUCHINJA KWA ASIE KUWA ALLAH

***Maana ya kuchinja:**
Ki lugha: Katika asili ni Mpasuko au mfano wa hilo.
Ki sheria: Kuondoa Nafsi na kumwaga Damu kwa kutukuza na kujikurubisha kwa njia maalum.

***Vigawanyo vya kuchinja:**
Vigawanyo vi tatu:
1: Vichinjwa vya kisheria.
2: Vichinjwa vya halali.
3: Vichinjwa vya kishirikina.

**1: Vichinjwa vya kisheria:**
Mfano:
1: Udhuhiya (kichinjwa cha siku ya Iddy kubwa).
2: Kichinjwa cha Nadhiri kwa ajili ya Allah.
3: Kichinjwa cha Hijja.
4: Kichinjwa cha fidia kwenye Hijja au Umra.
5: Kichinjwa cha Akika ya Mtoto alie zaliwa.
6: Kichinjwa cha sadaka ya kujikurubisha kwa Allah.
7: Kichinjwa kwa ajili ya kuwakirimu wageni.

**2: Vichinjwa vya halali:**
Mfano:
1: Kumchinja Ngamia kwa ajili ya kumuuza.
2: Kuchinja kwa ajili ya kula.

**3: Vichinjwa vya kishirikina:**
Mfano:
1: Kuchinja kwa ajili ya Sanamu.
2: Kuchinja kwa ajili ya Jini.
3: Kuchinja kwa ajili ya Makaburi.
4: Kuchinja kabla ya kuhamia kwenye nyumba mpya kwa ajili ya kinga kutokana na Majini.
5: Kuchinja wakati Baba harusi na Bibi harusi wanapo ingia ndani huku wakikanyaga damu ya kichinjwa.
6: Kuchinja kwa ajili ya Allah lakini anataja lisilo kuwa jina la Allah wakati wa kuchinja.

***Hitimisho:**
1: Kuchinja ni Ibda inayo muhusu Allah, haifai kuipeleka kwa asie kuwa Allah.
Na dalili kauli yake Allah Mtukufu: (Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote). (Al-An'aam: 162).

2: Kuchinja kinyume na asie kuwa Allah huzingatiwa ni Shirki kubwa, na mwenye kufanya hilo kalaaniwa,
Na dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Kalaaniwa na Allah Yeyote atakae chinja kwa ajili asiye kuwa Allah). Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

## KUWEKA NADHIRI KWA ASIE KUWA ALLAH

***Maana yake:**
Ki lugha: Kujilazimisha.
Ki sheria: Kuilazimisha Mtu nafsi yake kufanya jambo zuri lisilo kuwa lazima, kwakumtukuza alie wekewa nadhiri.

***Nadhiri ni Ibada kwa ajili ya Allah:**
Fahamu ya kwamba Nadhiri ni Ibada kwa ajili ya Allah pekeyake, haipelekwi kwa mwengine, na atakae ipeleka kwa mwengine kwa hakika amefanya shirki kubwa.
Amesema Allah Mtukufu: (Wanatimiza ahadi).
(Al-Insaan: 7).
Na yeyote atakae weka nadhiri kinyume na Allah haifai kwake kuitekeleza.

***Wakati gani Nadhiri inakuwa ni Shirki?:**
Binadamu atakapo ilazimisha nafsi yake kitu sio kwa ajili ya Allah kwakukitukuza na kujikurubisha, mfano:
1: Kama kusema ikiwa Allah atamponya mgonjwa wangu; basi kwenye kaburi la walii Fulani nitatoa mbuzi kadha au mali.
2: Nikipata Mtoto nitachinja kwa ajili ya walii Fulani kwenye kaburi lake.
3: Walii Fulani au Jini Fulani namuwekea nadhiri kuchinja vichinjwa vitatu.
4: Kuweka Nadhiri kwa ajili ya Masanamu.
5: Kuweka Nadhiri kwa ajili ya jua na mwezi.

## ISTIANA NA ISTIGHATHA NA ISTIADHA

***Maana zake:**
Istiana: Kutafuta msada.
Istighatha: Kutafuta kuokolewa, nako ni kuondoshewa shida.
Istiadha: Kutaka ulinzi.

***Dalili ya kwamba vitu hivi vitatu ni Ibada:**
1: Kutaka msada:
Kauli yake Allah Mtukufu: (Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada). (Al-Faatiha: 5).
2: Kutafuta kuokolewa:
Kauli yake Allah Mtukufu: (Mlipo kuwa mkimuomba msaada Mola wenu, naye akakujibuni). (Al-Anfaal: 9).
3: Kutaka ulinzi:
Kauli yake Allah Mtukufu:
(Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu). (An-Naas: 1).

***Hukumu ya kutafuta msada na kuokolewa na ulinzi kinyume na Allah:**
Imegawanyika katika sehemu mbili:
**1: Inayo faa:**
Yatakapo kamilika masharti manne:
**1: Sharti mbili zinafungamana na muombaji wa msada na kuokolewa na kulindwa:**
1: Isiwe ni katika mambo yanayo muhusu Allah pekeyake.
2: Awe kiumbe ni mwenye uwezo nayo.

**2: Sharti mbili zinafungamana na alie ombwa msada na kuokowa na kulinda:**
1: Awe hai.
2: Awepo hapo.

**2: Yakishirikina.**
Patakapo kosekana moja kati ya sharti zilizo tangulia.

## MAOMBEZI

***Maana yake:**
**Kilugha:** Ni chimbuko la alifanya maombi anafanya maombi fanya maombi utakapo jaalia jambo kuwa na vitu viwili, na viwili ni kinyume ya kimoja.
**Kisheria:** Kuwa katikati kwa Kupatanisha, Ima kuleta manufaa au kuondoa madhara.

***Vigawanyo vya uombezi:**
1: Uombezi wenye kukataliwa.
2: Uombezi ulio thibiti.

***Uombezi wenye kukataliwa:**
1: Maana yake: (Niule unao tafutwa kwa asie kuwa Allah katika mambo asio yaweza isipokuwa Allah).
2: Dalili yake:
Kauli yake Allah Mtukufu: (Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhaalimu). (Al-Baqara: 254).

***Uombezi ulio thibiti:**
1: Maana yake: (Niule unao tafutwa kutoka kwa Allah).
2: Sharti zake:
1: Idhini ya Allah kwa muombaji afanye maombi.
2: Amridhie kwenye kuomba na mwenye kuombewa.
3: Dalili yake:
Kauli yake Allah Mtukufu: (Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake?). (Al-Baqara: 255).
Na kauli yake Allah Mtukufu: (Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipo kuwa baada ya Allah kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia).
(An-Najmi: 26).

***Hukumu ya kutafuta uombezi kwa alie hai mwenye uwezo:**
1: Ikiwa utatafuta kutoka kwake jambo la kisheria au la halali analiweza: Ya faa; na ni katika mlango wa kusaidiana katika kheri.
2: Unatafuta kutoka kwake jambo ambalo hana uwezo nalo zaidi ya Allah, Hiyo ni shirki.

## KUYAZURU MAKABURI

Kumegawanyika katika sehemu tatu:

**1: Ziara ya kisheria:**

Nayo ni ziara ya makaburini kwa sababu ya:
1: Kukumbuka akhera.
2: Kuwatolea salam watu wa makaburini.
3: Kuwaombea dua.

**2: Ziara ya kibid'a:**

Inapinga ukamilifu wa Tauhidi (kumpwekesha Allah), nayo ni njia katika njia za shirki, mfano:
1: Kukusudia kumuabudu Allah kwenye kaburi.
2: Kukusudia kutaka Baraka kwenye makaburi.
3;Kuwapelekea Thawabu ukiwa makaburini.
4: Kufunga safari kwa ajili ya kuzuru makaburi.

**3: Ziara ya kishirikina:**

Ina kanusha Tauhidi (kumpwekesha Allah).
Nayo ni:
(Kufanya kitu katika namna za ibada kwa ajili ya mwenye kaburi).
Mfano:
1: Amuombe Yeye kinyume na Allah.
2: Atake msada na kuokolewa na mwenye kaburi.
3: Kuchinja na kuweka nadhiri kwa mwenye kaburi.
Namfano wa haya.

## UCHAWI

***Maana yake:**

Kilugha: Yaliyo fichikana na wepesi wa sababu yake.
Kisheria: Ni Ruqya na Hirizi na Madawa ya kulevya vinaathiri katika nafsi na mwili kwa kutaka kwake Allah.

***Vigawanyo vya uchawi:**

Vigawanyo aina mbili:
1: Shirki kubwa:
Ni ule ambao unakuwa kwa njia za Majini na Masheitwani wana waabudu na kujikurubisha kwao na kuwasujudia ili wawadhuru wanao wakusudia kuwaroga.

**2: Uovu na uadui:**

Ni ule ambao unakuwa kwa njia za Madawa ya kulevya na mfano wake, na njia nyingine kuuficha mkono na kufanya kiini macho.

***Hukumu ya mchawi:**
1: Ikiwa uchawi wake ni katika fungu la kwanza:
Yeye ni kafiri na huuliwa kwa kuritadi.
2: Ikiwa uchawi wake ni katika fungu la pili:
Sio kafiri, lakini huesabiwa ni muovu mfanya maasi, na huuliwa katika mlango wa kuondoa uovu, atakapoona jambo hilo kiongozi.

***Dalili ya kwamba uchawi ni ukafiri:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru).
(Al-Baqara: 102).
Yeyote atakae fanya hivyo au akajifundisha au kuuridhia amekufuru na ametoka katika Uislamu.

***Hukumu ya Nashira** (kuondoa uchawi kwa alie rogwa).
Kuna aina mbili:
1: Kuondoa uchawi kwa kutumia uchawi mfano wake:
Nayo ni haramu na ni katika matendo ya shaitwani.
2: Kuondowa uchawi kwa kutumia Dua na nyiradi na dawa za halali:
Jambo hili lafaa na wala hakuna tatizo lolote.

***Kuwaambia watu kuhusu wachawi na kuwa tahadharisha nao:**
Niwajibu kuwambia watu kuhusu wachawi na kuwatahadharisha kwa hilo; kufanya hivyo ni katika kuondoa munkar (jambo baya) na kuwanasihi Waisilamu.

***Alama za kumjua mchawi:**
Utapoona alama moja kati ya alama hizi kwa mmoja miongani mwa waganga fahamu ya kwamba ni mchawi bila shaka yeyote.
1: Anamuuliza mgonjwa jina lake na jina la Mama yake.
2: Anachukua athari ya mgonjwa (nguo, kiremba, kanzu, joho).
3: Kuandika Twalasimu.
4: Kuisomea twalasimu na hirizi yasiyo fahamika.
5: Wakati mwengine hutaka mnyama mwenye sifa maalum ili amchinje, wala hataji jina la Allah wakati wa kuchinja, wakati mwengine hupakaa damu sehemu ya maumivu kwa mgonjwa, au humtupa katika sehemu mbaya.
6: Kumpa mgonjwa hirizi zinakuwa na pembe nne kwa ndani kuna herufi na namba namba.
7: Huongea maneno yasiyo fahamika.
8: Hupewa mgonjwa karatasi ili aichome na ajifukize nayo.
9: Hupewa mgonjwa vitu azike aridhini.

# KUHANI NA ARRAF

***Maana ya Kuhani:**
Niyule anaye eleza mambo ya baadae kwa njia ya majini na mashaitwani.

***Maana ya Arraf:**
Niyule anae dai kujua mambo ya sasa kama kujua sehemu waliyo iba na vilivyo potea kwa njia ya siri.

***Kudai Elimu ya siri:**
Ni ukafiri; kwa sababu ya kuipinga Qur'ani
Amesema Allah Mtukufu: (Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipo kuwa Allah). (An-Naml: 65).

***Vigawanyo vya wanao elezea mambo ya siri:**
1: Yeyote anaye elezea mambo ya siri kwa njia ya majini huyu huitwa kuhani.
2: Yeyote anaye elezea mambo ya siri kwa kuchora mistari kwenye ardhi huyu anaitwa mpiga ramli.
3: Yeyote anaye elezea mambo ya siri kwa njia ya nyota huyo ni mnajimu.
4: Yeyote anaye elezea vilivyo ibiwa na kupotea kwa njia ya siri huyo ni arraf (anae dai elimu ya siri).

***Hukumu ya kwenda kwa Makuhani na Wajuzi na Wachawi:**
Imegawanyika katika sehemu mbili:
**1: Mwenye kuwaendea na akawauliza bila ya kusadikisha:**
Hukumu: Ni haramu na ni katika madhambi makubwa na haito pokelewa swala yake kwamuda wa siku 40.
Dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
(Yeyote atakae muendea arraf (anae dai elimu ya siri) akamuuliza jambo lolote haito kubaliwa kwake swala kwa siku 40).
Kapokea hadithi hii Imam Muslim.
Na makusudio ya swala yake haina malipo ndani yake.

**2: Mwenye kuwaendea na akawauliza na akawasadikisha:**
Hukumu: Amekufuru yalio teremshwa juu ya Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
Dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
(Yeyote atakae muendea arraf (anae dai elimu ya siri) au kuhani akasadikisha anayo yasema kwa hakika amekufuru yalio teremshwa juu ya Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake)).
Kapokea hadithi hii Maimamu wanne na Hakim.

## TWIYARA (kutuhumiyana mikosi au nuksi kwa kurusha ndege)

***Maana yake:**
Kilugha: Ni kutokana na kurusha ndege, nako ni kutarajia mazuri au kutuhumu mabaya kwa kitu Fulani.
Kisheria: Ni kutuhumu kunako sababishwa na kitu kinacho onekana au kusikika au kitu maalum.

***Hukumu ya Twiyara:**
Kutuhumu hupinga ukamilifu wa Tauhidi; na hilo nikwa sababu mbili:
1: Hakika mwenye kurusha ndege amekata mategemeo yake juu ya Allah na akategemea kisichokuwa Allah.
2: Hakika yeye kafungamana na kisicho kuwa na uhakika, ni udanganyifu na upumbavu.

***Dalili za kukataza Twiyara:**
Kauli yake Allah Mtukufu:
(Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Allah. Lakini wengi wao hawajui). (Al-A'araf: 131).
Nakauli yake Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Hakuna maambukizi, (maradhi kutoka kwa huyu kwenda kwa yule yenyewe bila kutaka Allah) wala kurusha ndege, (kuitakidi ikielekea upande wa kushoto safari itakua mbaya) wala Bundi (kuitakidi akilia juu ya nyumba yako kuna mtu atafariki) wala hakuna mdudu tumboni anae leta njaa, (waarabu walikua wakiitakidi ya kwamba kuna mdudu Fulani yupo tumboni anasababisha njaa)).
Kapokea hadithi hii Imam Bukharin a Muslim.
Na kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Kurusha ndege ni shirki). Kapokea hadithi hii Imamu Abuu Daud na Tirmidhy.

***Hali za wafanya Twiyara:**
Hazipunguwi hali mbili:
1: Ajiepushe na kukubaliana na kitendo hicho cha kurusha ndege na aache kufanya matendo, na hili ni miongoni mwa kujituhumu na kujipa nuksi.
2: Aende lakini akiwa na dhiki na tabu na masikitiko huku akichelea athari mbaya ya kurusha ndege, na hili linaunafuu kuliko la kwanza.
Na yote mawili ni upungufu katika tauhidi na madhara juu ya mja.

***Tiba kwa atakae kuwa na Twiyara (kujituhumu kuwa na nuksi) katika moyo wake:**
Aseme: (Allahumma la' ya'ti bilhasanati illa anta,wala yadfa' sayyiaha illa anta, wala haula wala quwwata illa Bika).
Kapokea hadithi hii Imam Abudaudi.

Maana yake: Ewe Allah hakuna anaeleta kheri isipokuwa wewe, wala anae ondoa shari ila wewe, wala hakuna mwenye hila ya kujiepusha na maasi wala nguvu ya kufanya mema isipokuwa kwa msaada wako.
Na ana sema tena: (Allahumma la' Twaira illa twairuka, wala' khaira illa khairuka, wala'ilaha ghairuka).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na kaisahihisha Sheikh Albani.
Maana yake: Ewe Allah hakuna kurusha ndege (nuksi, au jambo baya) isipokuwa hutoka kwako, wala hakuna kheri isipokuwa hutoka kwako, nawala hakuna Allah zaidi yako.

**Kisha ni juu yake:**
1: Kujua madhara ya kurusha ndege.
2: Kupambana na nafsi yake.
3: Kuamini alivyo hukumu Allah na makadara yake.
4: Kuwa na dhana nzuri kwa Allah.
5: Kutumia Istikhara.

***Kiwango cha Twiyara kilicho katazwa:**
Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
(Hakika ya kurusha ndege: kukikupeleka, au kukurejesha).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad.
Maana yake: Ndege itakaporushwa ikenda kushoto usiitakidi vibaya ikawa ni sababu ya kuvunja safari, au ikenda kulia ikawa ni sababu ya kufanya unacho kusudia, jambo hilo halifai kabisa yatakiwa umtegeme Allah pekeyake usiwe na itikadi potofu.

***Neno zuri:**
Maana yake: Neno zuri analo lisikia binadamu akafurahi nalo.
Mfano:
Mtu anataka kusafiri akamsikia anaesema: Ewe salim, akafurahi kwa hilo.
Kwa maana Salim ni jina zuri akafurahi kwa kusikia jina hilo.
Hukumu yake: Yafaa.
Dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Na hunipendeza neno zuri).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

***Tofauti kati ya kurusha Ndege na Neno zuri:**
Kurusha ndege ni kuwa na dhana mbaya kwa Allah, na kuhamisha jambo katika haki zake kwa mwengine, na kufunga mana moyo kwa kiumbe asiye nufaisha wala kudhuru.
Neno zuri: Nikuwa na dhana nzuri na Allah, hairejeshi mahitaji.

# KUTUMIA NYOTA

***Maana yake:**
Kilugha: Ni chimbuko la nyota, kwa maana kajifundisha elimu ya nyota au kuitakidi athari ya nyota.
Kisheria: Kutolea ushahidi kwa kupitia nyota kwa baadhi ya mambo.

***Vigawanyo vya Elimu ya Nyota:**
Vigawanyo viwli:
1: Elimu ya hukumu na kuathiri.
2: Elimu ya sababu na uendeshaji.

***Elimu ya hukumu na kuathiri:**
Vigawanyo vitatu:
1: Kuitakidi ya kwamba nyota zinauwezo wa kuathiri, (zinaumba matukio na mambo mabaya) jambo hili ni Shirki kubwa.
2: Kuzifanya nyota kuwa ni sababu ya kujua elimu ya siri: jambo hilo ni Shirki kubwa.
3: Kuitakidi ya kwamba nyota ni sababu ya kutokea kheri au shari, na Allah ndiye mtendaji: jambo hili ni haramu na Shirki ndogo.

***Elimu ya sababu na uendeshaji:**
Vigawanyo viwili:
1: Kutoa ushahidi kwa mwendo wa nyota katika mambo ya dini, jambo hili hutakiwa.
Mfano: kutoa ushahidi kwa kutumia nyota kwa kujua Kibla.
2: Kutoa ushahidi kwa kutumia nyota kwa mambo ya kidunia.
Nako kupo namna mbili:
1: Kutumia nyota kujua pembe za dunia:
(mashariki, magharibi, kusini, kaskazini) jambo hili lafaa.
2: Kutumia nyota kwa kujua misimu:
yafaa na wala hakuna karaha ndani yake.

***Faida: Hekima ya kuumbwa Nyota:**
Nazo ni tatu:
1: Nyota ni mapambo ya mbinguni.
2: Ni vimondo kwa Mashaitwani.
3: Na alama kwa ajili ya kufuata njia.

# KUPATA MVUA KWA SABABU YA NYOTA

***Makusudio yake:**
Kutafuta mvua.
Nyota: Ni wingi, na makusudio mapitio 28 ya nyota.
Na makusudio ya kupata mvua kwa sababu ya nyota:
Kuinasibisha mvua na nyota.

***Vigawanyo vya kupata mvua kwa sababau ya nyota:**
Vigawanyo vitatu:

**1: Shirki kubwa:**
Nayo ina namna mbili:
1: Aiombe nyota ili iteremshe mvua.
Kama kusema: Ewe nyota Fulani tupe mvua, Ewe nyota Fulani tuteremshie mvua.. na yanayo fanana na hayo.
2: Anasibishe kuteremka mvua kwa sababu ya nyota Fulani, ya kwamba yenyewe ndiyo iliyo teremsha bila ya Allah hatakama hakuiomba.

**2: Shirki ndogo:**
Nayo ni kujaalia nyota hizi kua ndio sababu.

**3: Yafaa:**
Nako ni kujaalia nyota hizo kuwa ni alama na dalili, wala sio sababu, wala hazina athari yoyote kwa mustakbali.

***Dalili ya kuharamisha kupata mvua kwa sababu ya nyota:**
Kauli yake Allah Mtukufu: (Na badala ya kushukuru kwa riziki yenu mnafanya kuwa mnakadhibisha?). (Al-Waqiah: 82).

Amesema Mujahid: Maana yake: Maneno yao kuhusu nyota: tumenyeshelezewa mvua kwa nyota Fulani na nyota Fulani.

Na kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Je! Mwajuwa kasema nini Mola wenu?) wakasema: Allah na Mtume wake ndio wajuzi. Akasema: (Wameamka katika waja wangu walio niamini mimi na walio nikufuru, ama yule alie sema: tumepata mvua kwa sababu ya Fadhila za Allah na Rehma zake, huyo kaniamini mimi kakufuru nyota, na ama yule aliye sema: tumepata mvua kwa sababu ya nyota Fulani na Fulani huyo kanikufuru mimi kaamini nyota).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

## RIYA (kujionyesha)

***Maana yake:**
Kilugha: Kudhihirisha kitu kwa mwenzako ili akione.
Kisheria: Kudhihirisha Ibada kwa mwengine ili watu waone na wamsifu.

***Hukumu ya Riya:**
1: Riya ndogo:
Shirki ndogo.
2: Kila matendo yake au yalio mengi ni riya:
Shirki kubwa, na hili halitokei kwa Muumini bali ni katika alama za wanaafiki.

***Hatari ya Riya:**
1: Yenyewe ni shirki ndogo.
Kasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Kitu ninacho kikhofia juu yenu ni shirki ndogo) akaulizwa kuhusiana nayo akasema: (Riya).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad.

2: Ya kwamba hatosamehewa ikiwa hatotubia muhusika:
Kwa kauli yake Allah Mtukufu: (Hakika Allah hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye) (An-Nisaa: 48).
Na hili linakusanya shirki kubwa na ndogo.

3: Yenyewe huarabu matendo yaliyo changanyikana na riya:
Kasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Kasema Allah Mtukufu: Mimi ni tajiri ya wale wanao nishirikisha na shirki zao, yeyote atakae fanya amali akanishirikisha na mwengine nitamuacha na shirki yake).
Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

4: Yenyewe ni kubwa zaidi kuliko fitna ya Masihiddajjal:
Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Jee! Nikwambieni ninacho hofia zaidi kwenu kuliko masihiddajjal?) wakasema ndiyo Ewe Mtume wa Allah. Akasema: (Shirki iliyo jificha, anasimama mtu anaswali, anaipamba swala yake, kwa sababu ya wale wanao mtazama).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad.

## MATENDO YANAPO INGILIWA NA RIYA

***Yana namna tatu:**
1: Msukumo wa kwanza nikuwaonyesha watu:
Hii ni shirki na Ibada hiyo ni batili.

**2: Iwe nia yake ni kwaajili ya Allah kisha ikaingia riya:**
Hili lina namna mbili:
1: Apambane na nafsi yake wala asiipe riya nafasi wala isikae kabisa, kwa kufanya hivyo hakuto haribika chochote.
2: Itulizane riya na kuipa nafasi nakuto iondowa.

**Na hukumu ya Ibada hapa:**
1: Ikiwa Riya aliyo ifanya haikusanyi Ibada zilizo tangulia.
Ibada za mwanzo zitakuwa sahihi; zilizo ingiliwa na Riya ni batili.
Mfano: Mtu katoa sadaka ya riyali(100) kwaajili ya Allah kisha akaona Mtu akatoa sadaka ya riyali (100) nyingine kwa kujionyesha, sadaka ya kwanza ni sahihi ya pili ni batili.
2: Ikiwa Riya aliyo ifanya inakusanya na Ibada zilizo tangulia.
Hapa Ibada zote hubatilika.
Mfano: Mtu kasimama kwa kusali rakaa mbili kwaajili ya Allah, ikaingia Riya kwenye rakaa ya pili wala hakuiondowa hiyo riya kaendelea nayo, hapa sala yote hubatilika.

**3: Inapo ingia Riya baada ya kumaliza Ibada.**
Haiathiri chochote.
Jambo: Yeyote atakae sikia watu wakimsifu kisha akafurahi kwa hilo: Hakuna chochote juu yake bali (Hiyo ni bishara njema kwa Muumini). Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

***Jambo: Yeyote atakae acha matendo kwa sababu ya watu:**
Kuacha amali kwa sababu ya watu ni riya.

***Tofauti kati ya Riya na Kusifiwa:**
Riya: Yahusiana na macho, maana yake:
(Anafanya mtu matendo ili watu wamuone na wamsifu).
Kusifiwa: Yahusiana na kusikia, maana yake:
(Anafanya mtu matendo ili watu wasikie na wamsifu).

***Tiba ya Riya:**
1: Kumbuka ubora wa Ikhlas; kufanya mambo kwaajili ya Allah.
2: Kumbuka madhara ya Riya na kwa hakika huharibu matendo.
3: Kumbuka Akhera.
4: Atambuwe ya kwamba watu hawamiliki manufaa wala madhara.
5: Dua, miongoni mwazo: (Allahumma Inniy audhubika an ushrika bika shaian wa ana a'lamu, wa astaghfiruka lima' la a;lamu).

Maana yake: Ewe Allah hakika mimi nina jilinda kwako na kuto kukushirikisha kwa chochote hali ya kujuwa, na nina kuomba msamaha kwa nisilo lijuwa.

## MWANADAMU KUFANYA IBADA KWA SABABU YA MASILAHI YA DUNIA

***Makusudio yake:**
Afanye mwanadamu ibada nyeti kabisa ili apate masilahi ya kidunia.

***Mifano kwa hilo:**
1: Kama anae fanya ibada ya Hijja ili achukuwe pesa.
2: Na kama anae pigana Vita ili apate ngawira.
3: Na kama anae adhini ili apate mshahara.
4: Na kama anae tafuta elimu ya sheria ili apate shahada na kazi tuu.

***Hukumu yake:**
Namna mbili:
1: Iwe asilimia kubwa ya matendo yake au yote ni kuitaka dunia;
Hili ni Shirki.
2: Afanye amali maalumu na akusudie kwa amali hiyo kupata dunia;
Hii ni Shirki ndogo inaharibu matendo.

***Onyo kwa mwanadamu kufanya kwake amali kwa kuitaka dunia:**
Amesema Allah Mtukufu:
(Wanao taka maisha ya dunia na pumbao lake tutawalipa humo vitendo vyao kaamili. Na wao humo hawatopunjwa* Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyo yafanya, na yatapotea bure waliyo kuwa wakiyatenda). (Hud: 15-16).
Na akasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae jifundisha elimu amabyo ndani yake ni kutafuta radhi za Allah, hajifundishi isipokuwa lengo lake apate dunia, hatoionja harufu ya pepo). Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Abudaudi.

## KUAPA KINYUME NA ASIEKUWA ALLAH

***Maana ya kuapa:**
Kilugh: Ina maana ya kulazimiana.
Kisheria: Kutilia mkazo hukumu kwa kumtaja mtukufu kwa kutumia herufi za kiapo:
Na herufi za kiapo ni: Wau, Be', Te'.

***Matamshi mengine:**
Na huitwa:
1: Yamin.
2: Kiapo.

***Kiapo cha kisheria:**
Nikile kilichokuwa:
- Kwa jina la Allah. (Mfano: WAllahi, WaBillahi, WaTAllahi).
- Au kwa jina miongoni mwa majina yake
(Mfano: WaRrahman, WaL-adhim, WaSsami'u).
- Au kwa sifa miongoni mwa sifa zake (Mfano: Naapa kwa Utukufu wa Allah, kwa Rehma za Allah, kwa Elimu ya Allah).

***Hukumu ya kuapa kinyume na Allah:**
Ni namna mbili:
1: Ikiwa anamtukuza kwa kiwango cha Ibada,
mfano kumtukuza kama anavyo mtukuza Allah au zaidi;
Hii ni Shirki kubwa.
2: Ikiwa anamtukuza lakini haifikii kiwango cha usawa wa kumtukuza Allah;
Hii ni Shirki ndogo.

***Dalili juu ya mwenye kuapa kinyume na Allah:**
Maneno yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae apa kinyume na Allah kwa hakika amekufuru au ameshirikisha).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Abudaudi na Tirmidhi.

***Mifano ya kuapa kinyume na Allah:**
1: Kuapa kwa jina la Walii.
2: Kuapa kwa utukufu wa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), au kwa utukufu wa Walii.
3:Kuapa kwa uhai wa Watu Fulani.
4:Kuapa kwa Amana au Utukufu.

***Ufupi wenye faida kwa hukumu ya kuapa:**
1: Ni haramu kuapa kinyume na Allah, na kufanya hivyo ni Shirki.
2: Ni haramu kuapa kwa jina la Allah kwa uongo, nacho ni kiapo chenye kuangamiza.
3: Ni haramu kuapa sana kwa jina la Allah, -japo ni ukweli-

ikiwa hakuna dharura yoyote; kitendo hicho nikuto muheshimu Allah Mtukufu.
4: Yafaa kuapa kwa jina la Allah ikiwa ni kweli na wakati wa shida.

***Kafara kwa mwenye kuapa kinyume na Allah:**
Aseme: (La'ilaha illa llah).
Dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae apa akasema katika kiapo chake: kwa jina la Lata na UZza, aseme: (La'ilaha illa llah). Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

## KUFANYA USHIRIKA, KATI YA ALLAH NA YEYOTE KATIKA VIUMBE VYAKE KWA KUTUMIA :(NA)

***Makusudio yake:**
Kiunga nisho cha (Na) kati ya Allah na yeyote katika viumbe vyake, katika jambo lolote atakalo ingizwa kiumbe ndani yake.

***Mifano yake:**
1: Akitaka Allah na wewe.
2: Namtaraji Allah na nakutaraji wewe.
3: Nategemea kwa Allah na kwako.
4: Sina zaidi ya Allah na wewe.
5: Bila ya Allah na Fulani ninge angamia.
Na mfano wa maneno kama hayo.

***Hukumu:**
Imegawanyika katika sehemu mbili:
**1: Ikiwa anaitakidi usawa:**
Hiyo ni shirki kubwa hata kama atatumia neno (kisha).
**2: Ikiwa haitakidi usawa:**
Hiyo ni shirki ndogo.

***Ilio sahihi kwenye matamshi haya:**
Yapo katika namna mbili:
1: Alete kionganishi cha (kisha) bila ya kuitakidi usawa.
Mfano aseme: Akitaka Allah kisha wewe,
Nimemtegemea Allah kisha wewe.
2: Aegemeze mambo yote kwa Allah:
Aseme: Akitaka Allah pekeyake, Nimemtegemea Allah pekeyake, na mfano wa maneno kama hayo,
na kusema hivyo ndio bora zaidi.

***Tofauti kati ya (Wau) na (Thumma) katika haya matamshi:**
Kionganishi cha (Na): kina maana ya kulingana na usawa.
Kionganisha cha (Kisha): kina maana ya kufuatia.

## NENO (LAU)

*Kutumia neno hili kuna namna tatu:
**1: Inajuzu:**
Atakapoleta neno (lau) kwa njia ya maelezo tu.
Mfano: Lau unge hudhuria darsa unge faidika.
Na dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Lau bila ya kutanguliza jambo langu hili, ningelirejea nyuma nikafanya hilo, nisingeli kuja na wanyama, na ningeli kuwa huru pamoja nanyi).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

**2: Inapendeza:**
Atakapoleta neno (lau) katika kutamani mambo ya kheri.
Mfano: Lau ningelikuwa na mali ningeliitowa sadaka.
Na dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), katika kisa cha watu wanne,
Alisema mmoja wao:
(Lau ningelikuwa na mali ningelifanya kama anavyo fanya fulani).
Maana yake ametamani kufanya kheri.
Akasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
(Yeye kutokana na nia yake malipo yao yatakuwa sawa sawa).
Kapokea hadithi hii Imam Ahmad na Tirmidhi.

**3: Haifai:**
Atakapoleta neno (lau) katika namna tatu:
**1: Kupingana na sheria:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Lau wengeli tut'ii wasingeli uliwa). (Al-Imran: 168).

**2: Kupingana na qadari:**
Dalili kauli yake Allah Mtukufu:
(Wangeli kuwa kwetu wasingeli kufa na wasingeli uwawa). (Al-Imran: 156).

**3: Kutamani shari:**
Na dalili yake hadithi ya watu wanne aliposema mmoja wao:
(Lau ningelikuwa na mali ningelifanya matendo ya fulani).
Yeye katamani kufanya shari.
Akasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake):
(Yeye kutokana na nia yake madhabi yao yatakuwa sawa sawa).

## KUTUKANA ZAMA

***Makusudio yake:**
(Kutukana na kulaumu na kuufanya ulimwengu mbaya ambao ni zama na wakati).

***Hukumu za kutukana zama:**
Zimegawanyika katika sehem tatu:

**1: Anakusudia mazungumzo bila ya kulaumu:**
Jambo hili lafaa.
Mfano: (Tumechoka na jato la siku hizi).
Na kauli ya watu wa Nabii Lut' (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Hii leo ni siku ngumu)!.

**2: Autukane ulimwengu ya kwamba wenyewe ndio ufanyao:**
Kama kuitakidi ya kwamba wenyewe ndio wapindua mambo kutoka katika kheri kwenda kwenye shari, jambo hili ni shirki kubwa.

**3: Autukane ulimwengu ya kwamba ndio sehemu ya mambo mabaya kwa upande wake pamoja na kuitakidi ya kwamba Allah ndie Mfanyaji:**
Jambo hili ni haramu na nikatika madhambi makubwa.

***Kutukana zama ni kumuudhi Allah Mtukufu:**
Amesema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Amesema Allah Mtukufu: Ananiudhi binadamu anautukana zama na Mimi ndie zama, naugeuza usiku na mchana).
Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.
Na maana ya: (Mimi ndie zama) Muendeshaji na Muhusika wake.

**Zinduo:**
Zama sio jina miongoni mwa majina ya Allah Matukufu.

## KANUNI MBILI ZENYE MANUFAA KATIKA MATAMSHI

**1: Ulazima wa kuchunga Ulimi kwenye maneno ya haramu:**
Kama kusengenya na umbea na uongo.

Na shirki: kama kuapa kwa asie kuwa Allah.
Kwa sababu mwanadamu huhesabiwa kwa kila kinacho tamkwa na mdomo wake:
(Hatamki neno isipokuwa karibu yake yupo mwangalizi tayari). (Qaaf: 18).

Na mwanadamu huenda akatoka katika Uislamu kwa sababu ya neno moja analo lisema, nilazima kuchunga na kudhibiti matamshi na maneno.

**2: Matamshi na maneno yenye kubeba maana ya ushirikina:**
Haifai kuyatumia; kwa sababu matumizi yake huchelea kuingia katika shirki, au ikawa ni mlango wa kuingilia katika ushirikina.

## BIDA' (UZUSHI)

***Maana yake:**
Kilugha: Ni kitu kilicho zushwa kisicho na mfano ulio tangulia.
Kisheria: Yaliyo zushwa katika Dini bila ya Dalili.

***Vigawanyo vya uzushi:**
**1: Kuzua katika mambo ya Ada:**
Kama kuzua mambo yaliyo vumbuliwa ya kisasa, na jambo hili lafaa; kwa sababu asili katika mambo ya ada yafaa.

**2: Kuzua katika Dini:**
Na hili ni haramu; kwa sababu asili yake ni kusimama.
***Vigawanyo vya kuzua katika Dini:**
Vigawanyo vi tatu:

**1: Uzushi wa kiitikadi:**
Nako ni kuitakidi kinyume na alivyo eleza Allah na alivyo eleza Nbii wake Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake).
**Mfano wake:**
Uzushi wa kufananisha au uzushi wa kukanusha sifa za Allah na uzushi wa kukanusha Qadari.

**2: Uzushi wa kimatendo:**
Nao ni kumuabudu Allah kinyume na alivyo amrisha mfano:
1: Kuanzisha Ibada isio amrishwa.
2: Au kuzidisha au kupunguza katika ibada ya kisheria.
3: Au kuleta Ibada ya kisheria kwa namna ya uzushi.
4: Au kuufanya muda maalum kwaajili ya ibada ya kisheria haliyakuwa sheria haikuweka muda maalum.

**Mfano:**
Kujengea makaburi, na sherehe tofauti, na mahafali yaliyo zushwa.

**3: Uzushi wa kuacha:**
Nao ni kuacha kwa halali au kuacha kinacho takiwa kufanyika kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allah kwa ibada.
**Mfano:** Kuacha kula nyama kwa sababu ya kujikurubisha zaidi kwa Allah, au kuacha kuoa kwa sababu ya kujikurubisha mbele ya Allah kwa ibada.

***Vigawanyo vya uzushi kwa kuzingatia hukumu yake:**
Vigawanyo viwili:
**1: Uzushi wa ukafiri:**
Unamtoa muhusika katika Uislamu.
**Mfano wake:**
Uzushi wa Mashia, na kusema ya kwamba Qur-ani ni kiumbe.

**2: Uzushi wa uovu:**
Hupata madhambi muhusika lakini hatoki katika Uislamu.
**Mfano wake:**
Uzushi wa nyiradi za pamoja, na uzushi wa kuuhusisha usiku wa nusu ya mwezi wa Shabani kwa ibada.

***Onyo kutokana na uzushi na kuujibu:**
Inatosha kwa hili Aya na Hadithi mbili.
1: Kauli yake Allah Mtukufu:
(Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini). (Al-Maaida: 3).
2: Kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae zua jambo katika Uislamu huu, jambo lisilo kuwemo, kwa hakika yatarejeshwa)
Amepokea hadithi Imamu Bukhar na Muslim. Na katika upokezi wa Imamu Muslim: (Yeyote atakaefanya matendo hamna ndani yake amri yetu kwa hakika yatarejeshwa).
3:Kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Na shari ya mambo ni yale yenye kuzushwa, na kila chenye kuzushwa ni bid'a, na kila bid'a ni upotevu, na kila upotevu utampelekea mtu katika moto).
Kapokea hadithi hii Imamu Muslim na Imamu Nnasai.

***Je! Upo uzushi mzuri na uzushi mbaya:**
Nani aliyeigawanya bid'a kwenye:
1: Bid'a nzuri.
2: Bid'a mbaya.
Kwa hakika ni kosa na kuchanganyikiwa na kwenda kinyume na kauli ya Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Kwa hakika kila bid'a ni upotevu) kwasababu Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake) amehukum ya kwamba bid'a zote ni upotovu, na huyu anasema: Siyo kila bid'a ni upotovu bali kuna bid'a nzuri.

***Sababu zinazo pelekea kuenea uzushi:**
1: Ujinga kuhusu mambo ya Dini.
2: Kufuata matamanio ya Nafsi.
3: Kushikamana na fikra na rai za watu.
4: Kujifananisha na makafiri.
5: Kutegemea hadithi za uongo zisizo kuwa na asili.
6: Utamaduni na mambo yasio ya sawa yasiyo na ushahidi katika sheria wala akili haikubaliani nayo.

***Kanuni mbili muhimu zinazo faidisha kujua uzushi na kuujibu:**
1: Asili ya ibada haifai kuitekeleza mpaka papatikane dalili ya kuamrisha jambo hilo.
2: Ibada yoyote ambayo palikuwa na uwezekano wa kuitekeleza zama za Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), pamoja na Maswahaba zake watukufu na hapakuwepo kipingamizi chochote, jambo hilo halifai kulitekeleza.

***Zinduo mbili muhimu:**
1: Amesema Imam Malik (r.h): Yeyote atakae zua jambo katika Uislamu akaliona ni zuri, kwa hakika amedai ya kwamba Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), amefanya khiyana katika kufikisha kwake ujumbe, kwa sababu Allah anasema: (Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini). Al-Maaida: (3). Jambo lolote ambalo halikuwa ni dini kipindi hicho, haiwezekani kipindi hiki likawa ni dini.
2: Amesema Sheikh Albany (r.h): Nilazima tufahamu ya kwamba Bid'a yoyote anayo ileta mtu kwenye dini tufahamu ya kwamba ni haramu, bid'a siyo kama wanavyo danganyika watu wengi ya kwamba ipo kwenye daraja ya karaha tu.

***Baadhi ya uzushi ulio enea kwanye jamii:**
1: Sherehe ya kuzaliwa Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), na kuzaliwa wengine.

2: Sherehe ya usiku wa Israi na Miiraji.
3: Sherehe ya usiku wa nusu ya Shabani.
4: Sherehe ya kuzaliwa (Bathdey).
5: Kutafuta Baraka sehemu na kwenye kumbu kumbu na kwa watu walio hai na walio kufa.
6: Nyiradi za pamoja.
7: Kusomewa Qur-ani roho za marehemu katika mahafali tofauti.
8: Kuhusisha mwezi wa Rajabu kufanya Umra na ibada maalum.
9: Kudhihirisha Nia ndani ya swala.
10: Kufanya Tawasul kwa kupitia watu Fulani na vyeo vyao.

***Vitabu vinavyo fiidisha katika kutambua uzushi:**
1: Tah-dhiru minal-Bid'a. Sheikh Ibn Ba'z (r.h).
2: Assunani wal-mubtadia't. Sheikh Muhammad Abdussalam Qushairy.
3: Albida' wal-muhdatha't wama la' aswla lahu. Hamud Matwar.
4: Al-ibda' fy madhwaril-ibtida'. Sheikh Ally Mahfudh.
5: Albidaul-hauliyya. Sheikh AbdAllah Tuwaijiry.

**Faida:**
Uhalisia wa kufuata hauwezi kukamilika isipokuwa matendo yawe sambamba na sheria katika mambo sita:

| * | Sharti ya kuiga | Mifano ya kinyume |
|---|---|---|
| 1 | Sababu | Kama anae swali rakaa 2 kwa sababu ya kunyesha mvua |
| 2 | Jinsia | Kama anae towa zakatul-fitri pesa |
| 3 | Kiwango | Kama anae swali magharibi rakaa 4 makusudi |
| 4 | Namna | Kama anae tawadha kuanzia miguuni na kumalizia usoni |
| 5 | Zama | Kama anae chinja udhuhiya kwenye Ramadhani |
| 6 | Sehemu | Kama anae fanya itikafu kwenye jangwa |

## KULINGANIA KATIKA TAUHIDI

Kulingania katika njia ya Allah ni jambo kubwa sana, na ubora wake ni mkubwa, na ndio kazi ya mitume, na ndio vibarua vya waja wema na vipenzi vya Allah.
Anasema Mwenyezi: (Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora). (An-Nahl: 125).
Na anasema Allah Mtukufu: (Sema: Hii ndiyo Njia yangu – ninalingania kwa Allah kwa ilimu – mimi na wanao nifuata). (Yusuf: 108).
Na anasema Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Na'pa kwa jina la Allah, laiti Allah akikuongozea japo mtu Mmoja, ni bora kwako kuliko ngamia wekundu). Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.
Na anasema Mume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake): (Yeyote atakae lingania katika jambo la uongofu, atapata malipo na malipo ya watakaofuata, hawata punguziwa chochote katika malipo yao). Kapokea hadithi hii Imam Muslim.

***Tauhidi ndiyo jambo la kwanza kulinganiwa:**
Jambo la kwanza na laulazima kufahamika na kutambulika na kufanyiwa kazi na kuwalingania watu kwenye jambo hilo ni Tauhidi.
Na dalili kauli yake Mtume (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), zama alizo mtuma Muadhi kwenda Yemen: (Liwe jambo la kwanza kuwalingania ya kwamba Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah pekeyake).
Na katika upokezi mwengine: (Wa mpwekeshe Allah pekee). Kapokea hadithi hii Imam Bukhari na Muslim.

***Miongoni mwa njia za kulingania katika Tauhidi:**
Hizi ni baadhi ya njia wengi wanaziweza na hakuna uzito ndani yake:
1: Kuchapisha Vitabu na Vipeperushi, vinavyo zungumzia Tauhidi na kuvigawa.
2: Kuwaambia Matajiri wafanya biashara washindane katika kuchapisha na kugawa Vitabu vya Tauhidi.
3: Kurikodi kanda au cd, ambazo zinabainisha na kulingania Tauhidi.
4: Kutowa mawaidha na khutba na mihadhara mbali mbali inayo zungumzia Tauhidi kwa mwenye kuweza, au kuwaalika masheikh.
5: Kuwafundisha watoto na watu wa nyumbani misingi ya Tauhidi, na kutoa zawadi kwaajili ya changamoto hiyo.

## VITABU MUHIMU VYA TAUHIDI

Hii ni orodha ya baadhi ya vitabu vya Tauhidi, ndugu yangu Muislamu nakuusia uwenavyo na kuvisoma, ili uzidishe elimu yako kwa upande wa dini, na ujuwe mbinu za kuokoka, na njia za kufaulu, njia ambazo atakae zipitia atafaidika na kufaulu, na atakae jiepusha na njia hizo atakula hasara na kuangamia.
Na ufahamu ya kwamba somo la Tauhidi na kujifundisha itikadi sahihi ndio msingi mkubwa wa elimu ya fiqh katika dini, walikuwa baadhi ya wanachuoni wakigawa Fiq-hi katika sehemu mbili kuu:

**1: Fiq-hi kubwa:**
Wanakusudia mambo ya Tauhidi na Itikadi.
**2: Fiq-hi ndogo:**
Wanakusudia Hukumu za Ibada na Muamala mbali mbali.
Sasa nijuu yako kusoma vitabu hivi:
1: Usulu Thalatha.
2: Qawa'idul-Arba'.
3: Kashfu shub-hati.
4: Kitabu Ttauhid.
**Vyote ni vya Sheikh Muhammad bin Abdul-wahab (r.h).**
5: Maj-Muatu Ttauhidi Nnajdiyya.
6: Fat,hul-Maji'd sharhi kitabu Ttauhid.
**Vya Sheikh Abdurrahman bin Hassani.**
7: Taisirul-Azizul-Hamyd.
**Cha Sheikh Sulaiman bin AbdAllah.**
8: Ma'rijul-Qabul.
9: A'lamu Ssunnatul-Manshura.
**Vyote viwili vya Sheikh Hafidhul-Hakamy.**
10: Al-qaulul-Mufyd Ala' kitabi Ttauhid.
11: Sherehe ya Aqidatul-Wa'sitwiyya.
12: Al-Qawaidul-Muth'la fy Swifati Llahi wa As-Ma'ihil-Husna.
**Cha Sheikh Muhammad ibn Swaleh Al-uthaimyn.**
13: Kitabu Ttauhid.
14: Al-Irshadu Ila' swahihil-I'tiqadi.
15: Sherehe ya Aqidatul-Wa'sitwiyya.
**Vya Sheikh Swaleh Al-fauzani.**
16: Aqidatul-Wa'sitwiyya.
**Cha Sheikhul-Islam Ibn Taimiyya.**
Aqidatu Ttwahawiyya na Sherehe yake.
**Cha Ibn Abil-Izzi Hanafy.**

***Na pupia kusoma Vitabu na Fat-wa za hawa Masheikh:**
1: Cha Sheikhul-Islam Ibn Taimiyya.
2: Na Mwanafunzi wake Ibnul-Qayyim.
3: Sheikh Muhammad bin Abdul-wahab na watoto zake Maimamu.
4: Sheikh Abdul-Aziz bun AbdAllah bin Bazi.
5: Sheikh Muhammad ibn Swaleh Al-uthaimyn.
6: Sheikh AbdAllah Jibrin.
7: Sheikh Swaleh Al-fauzani.
Na wengine tofauti na hawa wanao julikana kwa Tauhidi na Itikadi iliyo safi kabisa.

**MWISHO KABISA:**

Kwa kumalizia risala hii, napeleka Shukrani za dhati kwa Allah na kumshukuru sana kwa kutujaalia kumaliza kitabu hiki.

Pia nataraji ya kwamba nimechangia katika kuelezea ndani ya kitabu hiki mambo mengi yanayo husiana na Tauhidi kwa ufupi na kubainisha hukumu zake.

Kama ninavyo muomba Allah Mtukufu amlipe kheri kila ambaye atakaye changia katika kuchapisha kitabu hiki na kukisambaza.

Rehma na Amani za Allah zimuendee Nabii Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), pamoja na Familia yake na Maswahaba zake na Waisilamu wote watakao fuata mwenendo wake mpaka siku ya mwisho.

Aamyn.

# FAHARASI YA MADA

**Mada** **Ukurasa**

1: Utangulizi....2
2: Maaya ya Tauhidi....4
3: Vigawanyo vya Tauhidi....5
4: Faida muhimu....6
5: Umuhimu wa Tauhidi na Fadhila zake....6
6: La'ilaha illa Llah....9
7: Masharti ya La'ilaha illa Llah ....10
8: Kushahidilia ya kwamba Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yake), ni Mtume wa Allah....12
9: Shirki maana yake na vigawanyo vyake....13
10: Namna za Shirki kubwa ....13
11: Mifano ya Shirki kubwa na ndogo....14
12: Historia ya ushirikina....15
13: Hatari ya ushirikina na adhabu zake....16
14: Vitenguzi vya Uislamu....16
15: Kumkufuru twaghut....18
16: Misingi mi tatu....19
17: Ukafiri ....20
18: Unafiq ....22
19: Kupenda kwa ajili ya Allah na kuchukia kwa ajili ya Allah....23
20: Vigawanyo vya watu kwa yanayofaa katika haki zao kwa kuwapenda na kuwachukia....24
21: Uislamu....25
22: Nguzo za Uislamu....25
23: Imani....26
24: Nguzo za Imani....26
25: Ihsani....28
26: Mahusiano kati ya uislam imani na ihsani....29
27: Ibada....29
28: Kanuni muhimu katika tauhidi ya ibada....30
29: Vigawanyo vya mapenzi ....31
30: Khofu ....32
31: Kutaraji....33
32: Kutegemea....34
33: Dua....35
34: Ruqya....36
35: Hirizi....37
36: Kutaka baraka....38
37: Kanuni muhimu katika mlango wa sababu ....40
38: Tawasul....41
39: Kuchinja kwa asie kuwa Allah ....42

40: Kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allah....................................43
41: Istiana, istighatha, istiadha..................................................44
42: Maombezi.....................................................................45
43: Kuzuru Makaburi ............................................................46
44: Uchawi.........................................................................46
45: Kuhani na Arraf ..............................................................48
46: Twiyara (kutuhumiana mikosi)...........................................49
47: Kutumia nyota.................................................................51
48: Kupata mvua kwa sababu ya Nyota ......................................52
49: Riya..............................................................................53
50: Matendo yanapoingiliwa na riya..........................................54
51: Mwanadamu kufanya Ibada kwa sababu ya maslahi ya Dunia........55
52 : Kuapa kinyume na asiyekuwa Allah....................................56
53: Kufanya ushirika kati ya Allah na yeyote katika viumbe vyake kwa kutumia: (NA)............................................................................57
54: Neno lau........................................................................58
55: Kutukana zama................................................................59
56: Kanuni mbili zenye manufaa kwenye matamshi .........................60
57: Bid'a (uzushi)..................................................................60
58: Kulingania katika Tauhidi ..................................................64
59: Vitabu muhimu vya tauhidi.................................................65
60: Mwisho..........................................................................66